Nipashe
Jumanne Desemba 17, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581893
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
Nipashe digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710
LIKE & FOLLOW US
epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

UKURASA WA 3
**Mwili** wa mfanyabiashara aliyetoweka siku tano wakutwa ukiwa mochwari



UKURASA WA 3
**Watatu** mbaroni tuhuma kumuua kigogo wa CCM



UKURASA WA 4
RIPOTI MAALUMU -2
**Madarasa** chakavu yawaweka hatarini wanafunzi, walimu na elimu yao

# Mbowe: Msiogope

• **Mnyika** ahoji hoja za Lissu kutolewa nje ya ofisi... *Endelea Uk. 2*




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, kuhusu kukamilika kwa uchaguzi wa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza mwakani. Kulia ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Adolf Nduguru na Naibu Waziri TAMISEMI, Zainabu Katimba. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

UKURASA 19

## MIVUTANO YAKWAMISHA UPATANISHI DRC, RWANDA

OFISI ya Rais wa Angola Joao Lourenço imesema mivutano iliyojitokeza wakati wa mzungumzo ya upatanishi wa amani kati ...

## Wanafunzi 974,332 wapangiwa shule kidato cha kwanza

UKURASA 3

# Samia aagiza waliokula bilioni 67/- za zabuni wachunguzwe

UKURASA 2



**MICHEZO** FADLU AWAJIA JUU CS SFAXIEN UK.24
**MAONI,** UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwasili katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) kufungua Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Viongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Samia aagiza waliokula bilioni 67/- za zabuni wachunguzwe

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango ameagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kupiga 'darubini' ya kiuchunguzi kwa wakati wote kwenye matumizi ya mitandao na simu katika kuhamisha fedha za rushwa wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwakani.

Mbali na kuelekeza nguvu zaidi katika uchaguzi ujao, pia ameelekeza TAKUKURU kufanyia kazi Taarifa ya Ukaguzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa taasisi 44 za umma zilizokaguliwa mwaka 2022/23.

Dk. Mpango alikuwa akizungumza jana jijini Arusha, wakati alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa viongozi wa TAKUKURU. Makamu wa Rais alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, taarifa hiyo ya ukaguzi ya PPRA inaonesha zabuni 15 zenye thamani ya Sh. bilioni 67.27 zimetolewa kwa kutumia maelezo ya zabuni (tender specifications) yenye kubagua baadhi ya wazabuni.

"Wazabuni walichaguliwa na kupewa mikataba 25 yenye thamani ya Sh. bilioni 56.7 pasipo kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni. Aidha, majadiliano ya mikataba 23 ya taasisi saba, yenye thamani ya Sh. bilioni 64.5 yalifanyika bila kuwapo mpango wa mahojiano, yaani 'negotiation plan'.

"Lakini pia, mikataba 60 yenye thamani ya Sh. bilioni 54, ilitiwa saini pasipo kuidhinishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG). Na mikataba 10 ya ununuzi kwenye taasisi tano yenye thamani ya Sh. bilioni 7.48 iliongezwa muda bila kufuata utaratibu.

"Sasa yote haya yanadhihirisha kuwa katika taratibu za ununuzi vipo viashiria vikuu vya rushwa. Kwa hiyo ni vyema TAKUKURU ifanyie kazi taarifa hizi na kuchukua hatua stahiki," aliagiza.

Katika hotuba yake hiyo, Dk. Mpango alitaja maeneo tishio yanayotikisa kwa rushwa hivi sasa nchini kuwa ni sekta za ardhi, Jeshi la Polisi, rushwa kubwa kwenye ukusanyaji mapato ya serikali kuu na kwenye halmashauri na zabuni.

"Vitendo vya rushwa bado vinaonekana katika sekta mbalimbali hadi sasa, na yako maeneo mengi yanayotajwa. Kuna tatizo kubwa ardhi, kuna tatizo polisi, kuna rushwa kubwa ya rushwa kwenye kusanyaji wa mapato ya serikali kuu na kwenye halmashauri.

"Kuna upande wa zabuni, kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo, kuna rushwa kwenye upatikanaji leseni lakini pia upande wa uchaguzi na kadhalika.

"Na wananchi wetu bado wana malalamiko juu ya rushwa na kunyimwa haki. Taarifa za kila mwaka za TAKUKURU, lakini pia PPRA zinathibitisha," alisema.

Kbla ya Makamu wa Rais kuagiza hayo, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU nchini, Crispin Chalamila, alisema rushwa sasa ni tatizo la kidunia lenye madhara makubwa kwa mtu, jamii, nchi na kimataifa.

Alisema rushwa imetumika kupoka haki za watu kwa kumnyang'anya kwa mfano haki ya ardhi, yeye aliyestahili na kumpa yule asiyestahili, kwa sababu mwenye jukumu la kutoa haki amepokea fedha au kuahidiwa kupewa fedha akipindisha sheria.

"Uwezeshaji wa serikali tunaopata, umetuwezesha kwa mfano kuokoa fedha zaidi ya Sh. bilioni 18 kupitia operesheni mbalimbali za uchunguzi pamoja na ufuatiliaji miradi ya maendeleo," alisema Chalamila.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, akizungumza katika mkutano huo, alisema katika kipindi cha mwaka 2022/23-2024/25, TAKUKURU imepewa vibali vya ajira 1,190 vya watumishi wapya wa wilaya, mikoa na vituo maalumu kulingana na uhitaji.

Alisema taasisi hiyo pia imepewa magari mapya 195 yaliyogharimu Sh. bilioni 39.174, majengo ya ofisi 23 zenye thamani ya Sh. bilioni 12.5 na kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa kutandaza mfumo na kununua vifaa, jumla ya Sh. bilioni 3.446.

**Kwa maoni: +255 677 020 701**
**Email:customerrelations@guardian**

# Mbowe asema CHADEMA wasiogope

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amewataka wanachama wa chama hicho kutokata tamaa, bali wawe na roho ya ujasiri na kupambana.

Amesema misukosuko inayotokea ndani ya chama hicho isiwatishe bali ni sehemu ya maisha, akiendelea kusisitiza taasisi yoyote ni lazima ipitie katika misukosuko.

Mbowe alitoa kauli hiyo juzi jioni wakati akizindua ofisi ya CHADEMA Wilaya ya Kinondoni, mkoa wa Dar es Salaam.

"Kazi za siasa hazipaswi kukata tamaa, tusikubali kuingiza roho za ukataji tamaa, tuwe na roho za ujasiri wa kupambana, na tunapoingiza roho za kukata tamaa, ndipo tunaanza kutafutana uchawi, hatupaswi kutafutana uchawi.

"Tuna kila sababu ya kuimarishana, kujengana, kukumbatiana kuisaidia CHADEMA yetu ikawe bora zaidi. Na mimi kama mwenyekiti wa kipindi changu, nitahakikisha jambo hili ninalisimamia kwa nguvu kubwa sana," alisema Mbowe.

Mwenyekiti huyo pia aliwaomba viongozi na wanachama wa chama hicho kuendelea kusimamia nidhamu ya chama.

"Niwaombe viongozi wangu, nimesikia matamko mbalimbali kuhusu mambo ya nidhamu, jambo hili ni jema, kasimamieni nidhamu, na si tu kutukanwa Mbowe, kutukanwa kiongozi mwenzetu yeyote, hata angekuwa wa wilaya, wa jimbo, sisi lazima tuijenge familia, na familia haiwezi kuwa taasisi ya kutukanana, familia inakuwa taasisi ya kujengana na kutiana matumaini.

"Kasimamieni nidhamu, si kwa kuangalia sijui wewe ulimtukana Mbowe... hapana! Kwa kuangalia wewe ni kiongozi wa chama, huwatukani viongozi wenzako.

"Hata mnapotofautiana makosa au mitazamo, kawaone kama ni watu ambao wana haki hiyo, mrekebishane, mnyooshe mambo, taasisi hii ikawe imara zaidi," aliagiza Mbowe.

Mwenyekiti huyo aliwaambia wanachama wake hao wakati akizindua ofisi hiyo ya chama chake wilayani Kinondoni kuwa ni lazima waendelee kuishi kwa matumaini ili kulinda imani ya chama hicho, wakizingatia malengo ya chama chao.

"Wala misukosuko isiwatishe, ni sehemu ya maisha, ukishakuwa huna misukosuko kwenye taasisi, wewe ni mfu! Nimesema mara nyingi na nitarudia mara nyingi.

"Sisi chama chetu ni chama ambacho kinaishi, kinabadilika, kinatafuta mbinu mpya, tunamtafuta kila mmoja wetu, awe ni kijana ni mama, mzee, mtoto, kila mmoja wetu ana mchango na anapaswa kuwa wa mchango katika chama chetu.

"Kwahiyo tusikubali umoja wetu kama taasisi, tukatofautiana katika mawazo, tukaona yule aliwaza tofauti ana dhambi... hapana! Tutaendelea kujengana, kuimarishana, kusaidiana, kuongozana, kuonyana ili kwa pamoja tukaijenge CHADEMA yenye nguvu kesho kuliko ilivyo kuwa jana," alisema Mbowe.

Alisema chama hicho kwa sasa kimekuwa tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma, akiwataka wanachama kuendelea kukijenga na wasitoke kwenye mstari.

"Hiki chama awali kilikuwa ni cha watu wachache, leo kimekuwa ni chama cha kitaifa, wapo ambao ni wana CHADEMA, wapo ambao siyo wana CHADEMA, wote wanaona CHADEMA ndio tumaini pekee lililobaki katika taifa hili.

"Hawa watu tukiendelea kuimarika watakuja CHADEMA, hatimaye tutakuwa jeshi kubwa kuliko chochote kinachoweza kufikiriwa na hapo ndoto yetu ya kuliongoza taifa letu itakuwa inakwenda kutimia.

"Mungu awabariki, mkae kwa amani, mwendelee kukijenga chama, na kukilinda na kulindana wenyewe kwa wenyewe ili wote tusitoke kwenye mstari," alisema Mbowe.

**UCHUKUAJI FOMU**

Wakati huo, Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, jana alitangaza mchakato na ratiba ya uchaguzi wa chama ngazi ya taifa na mabaraza yake kwa kufungua dirisha la kuchukua na kurejesha fomu za kugombea nafasi mbalimbali kuanzia leo hadi Januari 5 mwakani.

Nafasi zinazogombewa ni za Mwenyekiti Taifa, Makamu Mwenyekiti Bara, Makamu Mwenyekiti Zanzibar, Katibu Mkuu Baraza la Wazee (BAZECHA) Bara, Naibu Katibu Mkuu Bara, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar na Mweka Hazina.

Wengine ni wajumbe watano wa Baraza Kuu ambao wanne kutoka Tanzania Bara na mmoja kutoka Tanzania Zanzibar, pamoja na wajumbe 20 wa Mkutano Mkuu ambao 15 kutoka Tanzania Bara na watano kutoka Tanzania Zanzibar.

Mnyika pia alitolewa ufafanuzi hoja za Lissu kuhusu uadilifu ndani ya chama, ikiwamo ya kupenyezwa fedha chafu, akitoa angalizo kuwa hoja za aina hiyo zilipaswa kutolewa kwa kufuata utaratibu wa ndani ya chama hicho badala ya ilivyo sasa - kutoa tuhuma nje ya utaratibu wao wa ndani.

"Nisisitize tu kama mtendaji mkuu wa chama, kwa nafasi yangu, ikiwa kuna kiongozi yeyote au mtu yeyote kwa maana ya mwanachama wa CHADEMA, ana tuhuma dhidi ya yeyote, aziwasilishe ili zishughulikiwe kwa mujibu wa katiba, itifaki na maadili ya chama na si kutoa tuhuma za jumlajumla, bila kusema kwamba 'hapa kuna huyu anatuhumiwa na hili na hili'.

Na katika hatua yoyote ile ya uendeshaji wa CHADEMA, tukipata tuhuma ambazo tunaona zina ushahidi wa kushughulikiwa, tutapeleka kwenye vikao vya kikatiba vya chama ambavyo kwa ngazi ya taifa.

"Tuhuma yoyote inayohusu mtu yeyote kwenye ngazi ya taifa, inapelekwa kwenye Kamati Kuu ya chama na yenyewe inaweza kuamua ama kushughulika na tuhuma hiyo yenyewe au kuikabidhi kwa Kamati ya Maadili ya Taifa ya chama," alisema.

**Kwa maoni: +255 677 020 701**
**Email:customerrelations@guardian**

# Mwili wa mfanyabiashara aliyepotea wakutwa mochwari

**Na Maulid Mmbaga**

ZIKIWA zimepita siku sita tangu kuripotiwa tukio la kupotea kwa mfanyabiashara, Daisle Ulomi, mkazi wa Mikocheni jijini Dar es Salaam, amekutwa amefariki na mwili wake kuhifadhiwa katika Hospitali ya Rufani Mwananyamala.

Ulomi alikuwa ni mfanyabiashara wa fedha za mitandao ya simu eneo la Sinza Kijiweni na Mwenge, alipotea katika mazingira yenye utata Desemba 11, mwaka huu alipomuaga mke wake anakwenda kufuatilia mzigo bandarini.

Akizungumza na Nipashe, baba mkwe wa Ulomi, Japhet Munisi, alisema mke wa marehemu alipigiwa simu jana kutoka hospitali na kuambiwa kwamba kuna mwili umeonekana uko katika chumba cha kuhifadhia maiti (mochwari).

Alisema, alikwenda, hospitalini na kuukagua mwili huo na kuutambua kuwa ni wa Ulomi.

"Tulipata taarifa hizi majira ya saa 7:00 mchana kwamba kuna mwili uko mochwari, ilibidi niende mimi Hospitali ya Mwananyamala kwa sababu ndugu wengine wako nje ya Dar es Salaam na nilithibitisha kuwa ni Ulomi, kwa sasa wanafamilia wanakaa kujadili kwamba atazikwa Moshi au wapi," alisema Munisi.

Aidha, baada ya kuthibitisha kuwa ni Ulomi aliwauliza wahudumu wa hospitali, lakini hawakutaka kumpa maelezo ya kina kwamba mwili huo ulifikaje eneo hilo.

"Niliwauliza askari waliokuwapo eneo hilo kwamba mwili wa Daisle umefikaje hospitali, wakasema wanafanya uchunguzi kwanza ndipo watatoa taarifa," alisema Munisi.

Taarifa zilizopatikana mitandaoni, zilieleza kuwa siku hiyo (Desemba 11), Ulomi aliondoka Sinza Kijiweni saa sita mchana, aliaga kuwa anakwenda Mbagala, bandari kavu kukagua kontena lake baada ya kuitwa na watu waliodai walikuwa wanashughulikia kulitoa bandarini.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa Ulomi aliondoka ofisini kwake akiwa na usafiri wa pikipiki akiendesha mwenyewe na tangu siku hiyo hakuonekana tena hadi mwili wake ulipopatikana akiwa amefariki.

Nipashe lilimtafuta Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro na alipopigiwa simu ilipokewa na msaidizi wake na kueleza kuwa kamanda (Muliro) yuko kwenye kikao, lakini kuhusu suala hilo uchunguzi unaendelea na utakapokamilika taarifa kamili zitatolewa.

# Wanafunzi 974,332 wapangiwa shule kidato cha kwanza

**Na Pilly Kigome**

WANAFUNZI 974,332 waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2024 wamechaguliwa kujiunga na shule za sekondari za serikali kuanza masomo ya kidato cha kwanza 2025.

Kati ya hao wasichana ni 525,225 na wenye mahitaji maalamu jumla ni 3,067.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alitangaza matokeo hayo jana alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari.

Alisema uchaguzi wa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka wa masomo 2025 umezingatia kigezo cha ufaulu wa mtahiniwa anayechaguliwa. Kila mtahiniwa aliyefanya mtihani na kupata jumla ya alama ya ufaulu kati ya 121 hadi 300 amechaguliwa na kupangiwa shule ya sekondari ya serikali.

Mchengerwa alisema, shule za sekondari walizopangiwa wanafunzi zipo katika makundi mawili za bweni na kutwa.

Za bweni zimegawanyika katika makundi matatu ambayo ni kwa wenye ufaulu wa juu, amali za kihandishi (ufundi) na bweni taifa ambazo zimepangiwa wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi kwa kuzingatia mgawanyo wa nafasi uliobainishwa na vigezo vilivyowekwa ili kuimarisha utaifa.

Shule za bweni kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu zimegawanya kila mkoa kulingana na idadi ya watahiniwa wa darasa la saba waliotahiniwa katika mkoa husika kwa kutumia kanuni ya kugawa nafasi hizo bila kujali idadi ya watahiniwa waliotahiniwa katika halmashauri.

"Shule hizo ni Msalato, Mzumbe, Kilakala, Ilboru, Tabora Girls na Tabora boys," alifafanua.

Nafasi za Shule za Sekondari za Amali za Kihandisi zimegawanywa kwa kila mkoa kulingana na idadi ya watahiniwa wa darasa la saba kwa mkoa husika kwa kutumia kanuni ya kugawa nafasi hizo kitaifa.

Shule hizo ni Tanga Tech, Moshi Tech, Musoma Tech, Bwiru Boys, Ifunda Tech, Iyunga Tech. Mtwara Tech, Mwadui Tech na Chato.

"Na vivyo hivyo mgawanyo wa nafasi katika shule za bweni kitaifa katika kila halmashauri kwa kufuata idadi ya watahiniwa kwa kutumia kanuni ya kugawa nafasi hizo," alisema.

Shule za wanafunzi wenye ufaulu wa alama za juu, jumla ya wanafunzi 809 wamechaguliwa kati yao wasichana 329 na wavulana 480.

Shule za Amali za Kihandisi jumla ya wanafunzi 1,174 wamechaguliwa, kati yao wasichana 197 na wavulana 977, shule za Bweni Taifa jumla ya wanafunzi 6,810 wamechaguliwa kati yao wasichana 5,199 na wavulana ni 1,611.

Kwa upande wa shule za kutwa jumla ya wanafunzi 965,539 wamechaguliwa kujiunga na shule za sekondari kati ya hao wasichana ni 519,500 na wavulana ni 446,039.

Aidha, alisema serikali ilifanya maandalizi mapema ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote watakaofaulu mtihani wa kumaliza darasa la saba mwaka 2024 wanajiunga na elimu ya sekondari ifikapo Januari 2025.

"Kutokana na maandalizi hayo wanafunzi wote 974,332 wataanza muhula wa kwanza wa masomo wa mwaka 2025 utakaoanza Januari 13, 2025," alisema.

Wakati huohuo, aliwataka wazazi na walezi kufanya maandalizi ya kutosha kwa watoto waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kuepuka kuchelewa kuripoti shuleni.

Pia, wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa, wakuu wilaya na wakurugenzi kuhakikisha maandalizi yote yanakamilika kwa wakati kupokea wanafunzi hao.



Katibu Mkuu wa Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Lucia Pande, akitoa salamu za mwaka kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, na kuelezea mafanikio na changamoto walizokutana nazo katika utendaji kazi kwa kipindi hicho chote. **PICHA: SABATO KASIKA**




# Watatu mbaroni tuhuma mauaji kada CCM

**Na Francis Godwin,** IRINGA

JESHI la Polisi mkoani Iringa linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za mauaji ya aliyekuwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa, Christina Kibiki.

Kada huyo aliuawa usiku wa kuamkia Novemba 13, mwaka huu, nyumbani kwake baada ya kuvamiwa na watu wasiojulikana.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Iringa, SACP Allan Bukumbi, alisema baada ya kutokea kwa kifo hicho waliendesha operesheni na kukamata watu mbalimbali ambao waliwahoji.

Kamanda Bukumbi alisema wanaendelea na msako wa kuwakamata watuhumiwa wengine na kwamba kuna baadhi watawakamata muda wowote kuanzia sasa upelelezi utakapokamilika na kufikishwa mahakamani.

Aidha, aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano wa kuwafichua wahalifu kwa kuwa ushirikiano wa Jeshi la Polisi na wananchi utasaidia kupunguza uhalifu.

Katika tukio lingine, Kamanda Bukumbi alisema Jeshi la Polisi mkoani humo linamsaka askari polisi Rogers mwenye namba F.4987 wa Kituo cha Polisi Ipogolo, pamoja na askari wa Jeshi la Akiba, Thomas Mkembela kwa tuhuma za kumuua Nashon Kiyeyeu (23), mkazi wa Nyamhanga, Kata ya Kitwiru, Manispaa ya Iringa.

Kamanda Bukumbi alisema mauaji hayo yalitokea Desemba 14, mwaka huu, na Sajenti Rogers kwa kushirikiana na mgambo walimkamata mtuhumiwa huyo kwa kuiba simu na kumpiga hadi kupoteza fahamu.

Alisema kuwa Sajenti Rogers alipokea taarifa kutoka kwa mwananchi mmoja ambaye hakumtaja jina kuwa anamtuhumu Nashon Kiyeyeu kumwibia simu, ndipo aliposhirikiana na mgambo huyo kumkamata.

Kamanda Bukumbi alisema baada ya kumkamata wanadaiwa walimpiga mtuhumiwa huyo hadi kupoteza fahamu na kumpeleka katika hospitali binafsi na kisha Hospitali ya Rufani ya Iringa, lakini baadaye alifariki dunia.

Alisema baada ya tukio hilo, askari na mgambo huyo walikimbia kusikojulikana na Jeshi la Polisi Mkoa wa Iringa linaendelea kuwasaka.

Akizungumza na waandishi wa habari, baba wa marehemu, Lusia Kiyeyeu alisema alipata taarifa za kukamatwa kwa mtoto wake kutoka kwa dada yake alikokuwa anafanya kazi.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa hizo alifuatilia kituoni hapo, lakini hakumkuta kijana wake wala askari aliyemkamata.

Kiyeyeu alisema baadaye aliienda Kituo Kikuu cha Polisi Iringa, lakini pia hakumkuta wala hakukuta jalada katika kituo hicho.

RIPOTI MAALUMU -2



Baadhi ya madarasa ya Shule ya Msingi Lipumba, wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma yalivyo sasa

# Madarasa chakavu yanavyowaweka hatarini wanafunzi, walimu na elimu

## -DED ajitetea mzigo mkubwa wa shule, bajeti haitoshi

**Na Mwandishi Wetu aliyekuwa**
MBINGA

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana, ilifafanua kwa kina ujirani wa madarasa chakavu ya shule na makaburi yenye miaka 90, unavyoathiri taaluma shuleni. Endelea na simulizi ya janga lingine la uchakavu wa madarasa na vyoo...**

---

MIUNDOMBINU shuleni imechakaa, hivyo usalama wa wanafunzi na walimu wao uko rehani. Watendaji wa serikali nao wanathibitisha kulitambua hilo, lakini utetezi wao bajeti iliyopo mikononi haikidhi kufanikisha ukombozi hivi sasa.

Hicho ndicho kilichoko katika Shule ya Msingi Lipumba, wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma. Imebeba jina linaloshabihiana na mwanasiasa na mtaalamu wa uchumi, Prof. Ibrahim Lipumba.

Shule hiyo ni zao la Azimio la Musoma na Operesheni Vijiji ya Mwaka 1974, lakini uhalisia ulioko shuleni haufanani na azimio hilo wala mahitaji ya kitaaluma.

Dhima ya Azimio la Musoma ni kuhakikisha kila mwananchi anapata elimu iliyo bora. Operesheni Vijiji ni nyenzo ya kuharakisha maendeleo kwa kuwapanga wananchi katika vijiji ili warahisishiwe utoaji huduma za kijamii, ikiwamo elimu.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Denis Malekano (54), anakiri shuleni kwake Lipumba kuna hali ngumu ya miundombinu iliyochakaa na haitoshi, akifafanua kuwapo vyumba saba vinavyotumiwa na wanafunzi 451 (wasichana 229). Kati yake, viwili vina hali mbaya, hata kuwaweka hatarini watumiaji wake, wanafunzi na walimu.

Anaendelea: "Vyumba vitano vinavyotumiwa na wanafunzi wa darasa la tatu hadi la saba, ni vibovu sana, vina nyufa! Tunajitahidi kutatua changamoto kwa kushirikiana na wanakijiji na halmashauri.

"Kuna darasa jipya lenye vyumba viwili na ofisi ya walimu linajengwa na wanakijiji. Halmashauri nayo inajenga darasa moja kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la awali. Fedha zilitolewa mwaka 2023/24," anasema Mwalimu Malekano, akifafanua madarasa yenye nyufa yalijengwa mwaka 1972, miaka 52 iliyopita.

Mwandishi wa habari hii amebaini madarasa hayo mbali na kuwa na nyufa, hayatoshelezi wanafunzi 451 waliopo; sakafu imebomoka na mahali pengine pana mashimo.

Plasta kwenye baadhi ya kuta imebanduka kiasi kwamba unaweza kuhesabu idadi ya matofali. Katika moja ya madarasa mlango umeshang'olewa na kuwekwa pembeni ndani ya darasa hilo; mabati ya paa yana kutu na ishara zote za kuoza.

Mwalimu Malekano anasema walimu kwa nafasi yao, wamekubaliana madarasa mawili yenye hali mbaya zaidi ya uchakavu, yasitumike ili kunusuru uhai wa wanafunzi na walimu, isipokuwa penye dharura ndipo wanalazimika kuyatumia.

"Kwa mfano, wakati wa Mtihani wa Taifa wa Upimaji Darasa la Saba Mwaka 2022, tulikuwa na wanafunzi 144. Tulihitaji vyumba sita. Hatukuwa na namna, tukayatumia (madarasa chakavu) hivyohivyo!

"Wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili wanatumia chumba kimoja cha darasa. La kwanza wanaingia darasani saa moja asubuhi hadi saa 5:30 asubuhi, wanawapisha darasa la pili ambao wanaosoma hadi saa 10:30 jioni," anasema.

**VYOO TAABANI**

Idadi hiyo ya wanafunzi 451 kutoka Shule ya Msingi Lipumba, wote wa kijiji hicho, wana shida nyingine ya pili inayohusu vyoo.

Viko katika hali mbaya inayokinzana na uhalisia wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (marejeo ya 2023) na maelekezo mbalimbali, yakiwamo mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya Machi 2017.

Mwalimu Mkuu Malekano anataja idadi ya matundu ya choo shuleni ni 12 (saba ya wasichana 229 na matano kwa ajili ya kaka zao 222). Vilevile, safu ya walimu na mkuu wao, wako 12, wanaotumia matundu mawili.

Mwandishi alishuhudia hali mbaya ya matundu hayo ya vyoo vya wanafunzi, uchakavu wa sakafu yake na kwa macho kuna viashiria vya kuporomoka wakati wowote. Kingine kinachokinzana na kanuni za afya na usalama, ni hali ya kuta zenyewe zilizojengwa kwa matofali ya kuchoma, zina kiashiria cha kubomoka.

"Hivi vyoo vilijengwa na wanakijiji, havikufikia viwango. Vimetitia mara nne; mara ya kwanza vilititia mwaka 2020. Bahati nzuri vilititia tukiwa likizo, hivyo havikuleta madhara kwa mwanafunzi yeyote. Mwaka 2021, 2023 na mwaka huu mwezi Februari vilititia tena. Hakuna mwanafunzi aliyedhurika," Mwalimu Mkuu anamfafanulia mwandishi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Lipumba, Mathias Mpangala, anadokeza hatua za tahadhari walizochukua kwa kiwango cha bajeti ya kijiji, wanawajengea matundu 14 ya vyoo vya wanafunzi, mradi unaoendelea sasa.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (marejeo ya 2023) inaelekeza kiwango kinachotakiwa shuleni ni kila tundu moja la choo litumiwe na wanafunzi 20 wa kike au 25 wa kiume.

Kwa mantiki hiyo, Shule ya Msingi Lipumba yenye wanafunzi 451, ina uhitaji wa matundu 11 kwa ajili ya wasichana 229 waliopo na tisa kwa wavulana 222. Hivyo, jumla ya matundu yanayohitajika sasa ni 20.

Sera tajwa pia inaelekeza uwiano wa madarasa na wanafunzi uwe darasa moja kwa wanafunzi wasiozidi 45. Hivyo, shuleni Lipumba kunahitajika vyumba 10 vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wake 451 waliopo.

**MAKAZI YA WALIMU**

Hali hiyo ndiyo inayotawala katika nyumba tatu za makazi ya walimu, akiwamo mkuu wao Malekano, ingawa zilijengwa na wanakijiji katika mwaka 1995 na 1999. Walimu wengine ni wapangaji kijijini na baadhi wako mjini Mbinga, umbali wa Km 18.1.

"Walimu tupo 12 (wanawake tisa). Wawili wamepanga kijijini Lipumba, umbali wa Km moja kutoka shuleni," anatamka Mwalimu Mkuu Malekano, akiwa na ufafanuzi kwamba walimu wanaoishi shuleni majirani zake wawili ni mwanamke na mwanamke.

Mwalimu Malekano analalamika kwamba, hata uhalisia wa makazi zinakopatikana nyumba hizo, hauendani na ramani rasmi zilizoelekezwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, akidokeza mabati yamechakaa na vyoo viko nje.

"Shule ina choo cha walimu cha kisasa chenye matundu mawili. Kilijengwa na wanakijiji mwaka 2010. Kabla ya hapo kulikuwa na choo chenye tundu moja kwa ajili ya walimu wote - wanaume na wanawake. Kilijengwa mwaka 1975 na wanakijiji. Mwaka 2009 kilititia," anafafanua.

Ofisa Elimu Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Veronica Justine anakiri kutambua uhalisia na madhira yanayowapata wanafunzi wake shuleni Lipumba, alikataa kutoa ufafanuzi kwa kauli: "Nikizungumzia suala hili nitakuwa ninakiuka taratibu. Msemaji wa halmashauri ni mkurugenzi."

Kwa upande wake, Msemaji wa halmashauri hiyo, Joseph Kashushura, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, anakiri na kuitolea maelezo kwamba: "Nina taarifa kuhusu changamoto ya miundombinu katika shule hiyo. Nina shule za msingi 168, nyingi zilijengwa zamani, majengo yake yamechakaa kama hiyo ya Lipumba.

"Bajeti haitoshi kufanya maboresho kwa shule zote kwa wakati mmoja. Tunajitahidi kujenga miundombinu mipya na kuboresha iliyopo kwa kadri ya bajeti inavyopatikana."

***ITAENDELEA KESHO**

**Kwa maoni: +255 677 020 701**
**Email:customerrelations@guardian**

# Mkurugenzi Jatu adai amekubaliana na walalamikaji kesi dhidi yake iishe

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Mkurugenzi wa Jatu, Peter Gasaya (33), anayekabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi kwa kujipatia Sh. bilioni 5.1 kwa njia ya udanganyifu, amedai mahakama kuwa wamekubaliana na walalamikaji kesi hiyo iishe.

Hivyo, anaomba mazungumzo na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ya yeye kukiri kosa yaendelee.

Gasaya alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Geofrey Mhini wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia.

Wakili wa Serikali, Frank Lomuli alidai kesi hiyo ilitwa kwa ajili ya kutajwa, upelelezi haujakamilika na akaomba tarehe nyingine ya kutajwa kwa kesi hiyo.

Baada ya kudai hayo, mshtakiwa alipewa nafasi azungumze. Alidai kuwa awali alipokuwa kwenye makubaliano (plea bargaining) alizungumza na walalamikaji wakakubaliana kwamba kesi hiyo iishe, kwahiyo anaomba yaanze upya.

Wakili Lomuli alidai makubaliano hayo yalishindikana na pia inawezekana makubaliano hayo kuanza, lakini hadi upelelezi ukamilike kwanza ndipo wataingia katika makubaliano hayo.

Hakimu Mhini aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba 30, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia, hivyo mshtakiwa ataendelea kukaa rumande.

Mshtakiwa Gasaya anadaiwa kuwa kati ya Januari Mosi, 2020 na Desemba 31, 2021, jijini Dar es Salaam, akiwa Mkurugenzi wa kampuni hiyo, alijipatia Sh. 5,139,865,733 kutoka Saccos ya Jatu kwa njia ya udanganyifu, jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

Ilidaiwa kuwa alijipatia kiasi hicho cha fedha kwa madai ya kuzungusha na kukizalisha kiasi hicho kwa kuwekeza katika mazao ya kilimo na kupata faida zaidi, jambo ambalo alifahamu si kweli.

Mshtakiwa Gasaya anatuhumiwa kutakatisha fedha hizo zilizokuwa katika akaunti ya Jatu iliyoko benki ya NMB Tawi la Temeke kwa kujirushia katika mitandao ya simu (miamala).

Inadaiwa kuwa mshtakiwa huyo alifanya hivyo huku akijua fedha hizo zinatokana na kosa tangulizi la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

# Uwekezaji TPA wavutia meli za kigeni

**Na Joseph Mwendapole**

UWEKEZAJI uliofanywa na Mamlaka ya Bandari (TPA) katika Bandari ya Mtwara umevutia meli nyingi za kigeni katika usafirishaji wa korosho kwenda katika masoko ya kimataifa na kuufanya msimu wa 2024/2025 wa zao hilo la biashara kuwa wa mafanikio.

Mafanikio hayo yanatokana na maboresho ya bandari hiyo yanayofanywa na serikali katika kusaidia ukuaji wa biashara ya korosho zinazozalishwa katika mikoa ya Kusini kwenye masoko ya kimataifa.

Mmoja wa wafanyabiashara wa korosho mkoani Mtwara, Omega Makanjiro, alisema jana kuwa uwekezaji huo umewezesha meli tatu kuhudumiwa kwa wakati mmoja katika gati mpya na ya zamani, jambo lililochangia na kampuni nyingi za meli kupeleka meli zao katika Bandari ya Mtwara na wafanyabiashara kusafirisha biashara zao kwa urahisi.

Aliipongeza TPA kwa juhudi za kuboresha huduma katika bandari hiyo na kuishauri iendelee kuitangaza kutokana na huduma zake zilizoboreshwa ili kuvutia kampuni nyingine za meli zaidi.

Naye Herman Colman kutoka kampuni ya ETG, alisema msimu huo umekuwa mzuri zaidi kwao, kwa kuwa tangu kuanza kwa msimu huu wameshasafirisha tani 40,000, ikilinganishwa na 26,000 walizosafirisha katika msimu uliopita.

"Hii inatokana na uboreshaji wa huduma na uwapo wa meli za kutosha katika kutoa huduma tunachukua na kusafirisha mizigo yetu kwa wakati na hii inapunguza gharama kwa mteja, ambaye ndiye mtumiaji wa mwisho," alisema.

Aliipongeza TPA kwa kuongeza mitambo na mashine za kisasa, jambo lililoongeza ufanisi na uwezo wa kuhudumia shehena nyingi kwa wakati.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania, Francis Alfred, alithibitisha kuwa uzalishaji wa korosho umeongezeka mwaka huu na hadi sasa, wameuza tani 238,000.

Aliongeza kuwa hakuna changamoto yoyote ya meli au makasha ya kubeba korosho kwa msimu huu, tofauti na misimu ya nyuma.

Alisisitiza kuwa ushirikiano wa karibu kati ya wanunuzi na wasafirishaji ni muhimu ili kuhakikisha msimu huu unakuwa endelevu katika kuunga mkono juhudi za serikali za kuinua hali za wakulima.

Taarifa ya TPA ilisema kuwa hadi mwishoni mwa mwezi Novemba 2024, TPA kupitia Bandari ya Mtwara imeshahudumia shehena ya korosho ghafi tani 133,000 kwa ajili ya masoko ya kimataifa, ongezeko kubwa la tani 72,921, ikilinganishwa na tani 60,079 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023 na kwa mujibu wa TPA, hili ni ongezeko la asilimia 121.

Taarifa ya TPA imeongeza kuwa meli 17 tayari zimefika na kuhudumiwa katika Bandari hiyo na kati ya hizo, 14 zimepakia shehena ya makasha (Container Vessels), huku tatu zikibeba korosho zilizopakiliwa kwa magunia.

Taarifa hiyo ilisema kuwa jumla ya makasha 3,366 tayari yamepakiliwa na kuondoka kutoka Bandari ya Mtwara, kati ya makasha 7,621 yaliyopo katika bandari hiyo kwa ajili ya kubeba zao hilo la biashara.

Ilisema serikali imewekeza zaidi ya Sh. bilioni 157.8 kuboresho Bandari ya Mtwara na mafanikio hayo ni sehemu ya matokeo ya uwekezaji huo.

Ilisema kabla ya uwekezaji huo, korosho zote kutoka mikoa ya Kusini zililazimika kusafirishwa kwa malori hadi Dar es Salaam ili zisiweze kusafirishwa kwenda masoko ya kimataifa.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA FEDHA**

**MWALIKO KWA WADAU WA KUSHIRIKI KATIKA SHUGHULI ZA KIKOSI KAZI CHA MABORESHO YA SERA ZA KODI (TASK FORCE ON TAX REFORMS) KWA AJILI YA MATAYARISHO YA BAJETI YA 2025/26**

Kamati ya Maboresho ya Sera za Kodi (Task Force on Tax Reforms) inayohusika na matayarisho ya Bajeti ya Serikali 2025/26 itaanza kazi yake mwezi Februari 2025. Vikao kazi vya Kamati vitazinduliwa na Kongamano la Kodi na Uwekezaji Kitaifa ambalo litafanyika mwezi Januari 2025.

Kila mwaka, Kamati hii, imekuwa ikipokea maoni ya wadau, kufanya uchambuzi, na kufanikisha majadiliano ya masuala mbalimbali yanayohusiana na sera za kodi na usimamizi wake. Maoni hayo yamekuwa na mchango mkubwa katika uandaaji wa sera na yamesaidia katika kuunda mfumo wa kodi ambao umewezesha utatuzi wa masuala mbalimbali ya kodi kwa ufasaha na uwazi.

Malengo ya sera za kodi kwa mwaka 2025/26 ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuvutia uwekezaji; kuwezesha ukuaji wa biashara ndogondogo na za kati kwa ukuaji endelevu wa uchumi; kuimarisha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari; upanuzi wa wigo wa kodi; kuongeza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika usimamizi wa kodi; kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi; na kuweka utaratibu mzuri wa ulipaji wa ada na tozo mbalimbali.

Ili kufanikisha kazi hiyo, Kamati inakaribisha ushiriki wa taasisi za Serikali, sekta binafsi, asasi zisizo za Serikali, taasisi za dini, jamii ya wasomi, taasisi za utafiti na wataalamu wengine katika sekta ya uchumi kwa kutoa maoni ya kuboresha sera za kodi kwa maandishi. Maoni hayo yanapaswa kuonesha yafuatayo:

i. Biashara, kampuni, taasisi, chama/vyama au makundi ambayo yanawakilisha;
ii. Mapendekezo ya mabadiliko ya kisera na mapato ya Serikali yanayotokana na kodi na yasiyo ya kodi, ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa sekta, maeneo au aina ya walipakodi ambao wataathirika, na kwa namna watakavyoathirika;
iii. Makisio ya athari kwenye uchumi na mapato ya Serikali katika mwaka huu wa utekelezaji na katika miaka ijayo;
iv. Sababu za mapendekezo ya mabadiliko kwenye sera za mapato, hususan uchambuzi wa namna ambavyo mapendekezo hayo yataisaidia Serikali kufanikisha malengo yake makuu; na
v. Pale ambapo mapendekezo yanapunguza mapato ya Serikali (hata katika kipindi cha muda mfupi), mapendekezo hayo yaoneshe bayana hatua za kufidia upungufu wa mapato ambao utajitokeza.

Kamati inatarajia kupata mapendekezo yatakayowezesha majadiliano yenye tija kati ya Serikali na Wadau.

Mapendekezo yawasilishwe kuanzia tarehe ya tangazo hili hadi tarehe **31 Machi 2025** kupitia lango (portal) lifuatalo: **https://maoni.mof.go.tz/. Maoni yatakayowasilishwa baada ya tarehe ya mwisho hayatapokelewa.**

Mapendekezo yanaweza pia kuwasilishwa kwa anuani ifuatayo:
**Sekretariati ya Kamati ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi,**

**Wizara ya Fedha,**
**Idara ya Uchambuzi wa Sera,**
**Jengo la Hazina (Ghorofa ya Pili),**
**18 Barabara ya Jakaya Kikwete,**
**S.L.P 2802,**
**DODOMA.**
**AU**
Barua Pepe: **mathias.kadebe@hazina.go.tz au salha.mzee@hazina.go.tz**

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na Mathias Kadebe 0713 694 895; au Salha Mzee 0652 442 944.
Pia tembelea tovuti yetu: www.mof.go.tz.

**Tangazo hili limetolewa na:**

**KATIBU MKUU - HAZINA**
**Desemba, 2024**

218298402

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Nchi za Afrika zijiimarishe masoko ya kimataifa

**MACHI** 21, 2018, nchi za Afrika zilitia saini mkataba wa makubaliano ya Eneo Huru la Biashara (AfCFTA), ambalo linakadiriwa kuwa na watu zaidi ya bilioni 1.2 na pato la dola za Marekani trilioni 2.5 kwa mwaka.

Vipo vigezo ambavyo vitawawezesha wafanyabiashara wa Tanzania kulifikia soko hilo na masoko mengine ya kimataifa ambayo yanaruhusu nchi nyingine kuuza huduma na bidhaa zake nchini.

Moja ya kigezo ni kuwa na biashara iliyosajiliwa ambayo inatunza kumbukumbu zake za kifedha, mauzo, ununuzi, uzalishaji (kwa wenye viwanda), na namna wafanyabiashara wanavyozingatia ajenda ya dunia ya maendeleo endelevu kwa sekta zote.

Hapa nchini, zipo mamlaka na taasisi zinazoratibisha masuala ya biashara na kuthibitisha uhalali wake, ambazo ni muhimu wananchi wazitumie kikamilifu ili AfCFTA na masoko mengine yawanufaishe Watanzania.

Moja ya taasisi hiyo ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ambayo inasajili kampuni, majina ya biashara, nembo za biashara, leseni za viwanda, miliki ubunifu na uvumbuzi (hataza).

Takwimu za BRELA zinaonyesha kwamba ni Watanzania wachache wanaomiliki biashara changa, ndogo na za kati wanaoona umuhimu wa kuzisajili. Kibaya zaidi ni kwamba ni wavumbuzi wachache zaidi, wanaojisajili kwa wakala huo.

Jambo la kusikitisha ni kwamba gharama za kujisajili zinahimilika ukilinganisha na hasara ambayo mtu anaweza kuipata kwa kutoilinda biashara yake kisheria.

Mathalani, kiwanda kidogo chenye mtaji wa chini ya Sh. milioni 10, kinachosindika unga, viungo au kinazalisha mafuta kinasajiliwa kwa Sh. 50,000 inayolipwa mara moja tu katika uhai wake wote.

Kwa wavumbuzi, ada ni Sh. 22,000 inayolipwa kwa awamu mbili na Sh. 4,000 kila mwaka baada ya kusajiliwa. Hiki ni kiasi kidogo ambacho bila shaka, Mtanzania mwenye nia ya kufanyabiashara kwa uaminifu, anamudu kuilipa.

Kama tunavyofahamu, mazingira ya Afrika kwa maana ya changamoto zinazoikabili jamii zinafanana kwa kiasi kikubwa; inasikitisha kuona mtu anabuni kitu kinachoweza kutatua changamoto kwenye jamii, anakiweka mtandaoni, anakipa na jina, bila kulinda jina wala uvumbuzi wenyewe.

Hali ni hiyo hiyo wakati wa maonyesho ya biashara kama ya Kimataifa ya Sabasaba ambayo yako mbioni kuanza; unakuta mbunifu anaeleza hatua kwa hatua namna alivyofanikiwa kubuni zana fulani ya kuwasaidia wakulima au wananchi katika sekta muhimu, baada ya maonyesho hanufaiki na ubunifu wake kwa kuwa wajanja wachache wanaamua kwenda kuisajili BRELA na kuanza kuizalisha. Hii ni hasara sio kwake pekee bali kwa nchi pia.

Mpango wa serikali wa kuboresha mazingira ya biashara nchini umeweka njia rahisi za kujisajili ambayo ni kupitia mtandao (ORS), unapata huduma zote za kurasimisha biashara yako ukiwa sehemu yoyote yenye intaneti.

Tunaeleza haya ili kuukumbusha umma kwamba wajasiriamali wetu wanaweza kuzalisha bidhaa nzuri, kutoa huduma bora, tukajitangaza mtandaoni lakini mwisho wa siku, tutakuta kile tunachouza kimelindwa kisheria na mtu mwingine; ambaye atakuruhusu kuendelea kutumia nembo au jina ulilobuni, kwa kumlipa mamilioni ya fedha kwa kuwa tu ameshajisajili.

Sheria itamlinda ambaye ameitii. Hata kama utakuwa mwanzishili wa huduma, jina, uvumbuzi au nembo, usipoisajili halafu akatokea mgeni akaisajili nchini, hutaweza kujitetea kwa sababu hutambuliki kwenye mifumo ya kisheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Sekondari hizi zisihujumiwe

**SERIKALI** inaendelea na juhudi za kujenga shule za sekondari za wasichana za masomo ya sayansi na hisabati kila mkoa ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo hayo.

Lengo la kufanya hivyo ni kutokana na baadhi ya wanafunzi wa kike, kuyakimbia masomo hayo kwa maelezo kwamba ni magumu, hatua iliyoifanya serikali kuamua kuja na mkakati huo.

Wakati kukiwa na jitihada hizo, baadhi ya watu wameanza kufanya hujuma ambazo huenda zikasababisha lengo la serikali kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo hayo kukwama.

Kuna hujuma ziliwahi kutangazwa na vyombo vya habari kuwa mifuko zaidi 600 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni 15, inayodaiwa kuwa ni ya ujenzi wa sekondari ya wasichana ya mkoa wa Mara ilikutwa katika nyumba ya mtu.

Shule hiyo inajengwa eneo la Bulamba, Halmashauri ya Wilaya Bunda, na kwamba semeti hiyo ilikuwa imepelekwa nyumbani kwa mhusika huyo anayeishi katika Kijiji cha Karukekere wilayani humo.

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Dk. Vincent Anney, anashuhudia mifuko hiyo na kusema tukio hilo ni la aibu na halikubaliki, huku akithitibisha kuwa amejiridhisha kwamba saruji hiyo ni mali ya serikali.

**Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Dk. Vincent Anney, anashuhudia mifuko hiyo na kusema tukio hilo ni la aibu na halikubaliki, huku akithitibisha kuwa amejiridhisha kwamba saruji hiyo ni mali ya serikali.**

Katika uthibitisho wake anasema saruji hiyo ni mali ya serikali, kwa kuwa miradi ya serikali inajengwa kwa saruji yenye kiwango cha ubora wa 42.5, tofauti na ile saruji ya mtaani ambayo ni 32.5.

Je, katika mazingira hayo ya hujuma, ni kweli miradi ya ujenzi wa sekondari hizo utakamilika kwa kiwango kinachotakiwa? Naona iko haja kwa serikali kufuatilia kwa karibu ujenzi wa sekondari hizo.

Inawezekana kukawa na hujuma ya aina hiyo au zaidi katika mikoa mingine inayotekeleza mradi wa ujenzi wa sekondari za mkoa kwa ajili ya masomo ya sayansi kwa wanafunzi wa kike.

Hivyo, kama inawezekana, kuwe na ufuatiliaji wa karibu wa ujenzi wa sekondari hizo katika mikoa yote ili kubaini kama hakuna hujuma ili kuhakikisha inatekelezwa kwa kiwango kinachotakiwa.

Inawezekana pia mikoa mbalimbali imeshakamilisha ujenzi wa sekondari hizo, lakini kwa hujuma za miradi ya maendeleo ambazo hujitokeza, ni vyema ukawapo ufuatiliaji wa kina.

Hatua hiyo itasaidia kuwafanya wanafunzi hao kusomea katika mazingira bora na salama, bila kuwapo hofu ya majengo kujengwa chini ya kiwango kwa sababu ya ubadhirifu wa saruji au vifaa vingine vya ujenzi.

Kikubwa zaidi ni kushirikisha wananchi katika hatua zote za awali za mradi hadi umaliziaji ili nao waweze kuufuatilia na kutoa taarifa iwapo kutakuwa na dalili za hujuma zozote watakazobaini.

Ninaeleza hivyo kwa sababu sekondari hizo ni za umma, kwani umma ni wananchi wenyewe ambao wanapaswa kujua miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao ili waweze kuilinda.

Hujuma katika miradi inayotekelezwa na serikali isiwe sehemu ya kawaida katika maisha ya kila siku. Kama ambavyo ilidhibitiwa katika ujenzi wa shule za msingi, ilidhibitiwe pia kwenye ujenzi wa sekondari hizo za masomo ya sayansi kwa ajili ya wasichana.

Miaka ya nyuma ilikuwa ni kawaida kuona ujenzi wa madarasa ya shule za msingi ukitekelezwa chini ya kiwango, kwani kuta zilikuwa zikipasuka baada ya ujenzi au sakafu kuharibika huku mabanzi yakitumika kupanua, lakini sasa hilo limeisha.

Tanzania itajengwa na Watanzania wenyewe, hivyo ni muhimu kuzingatia uzalendo badala ya kutanguliza ubinafsi au ulaji ambao mwisho wake ni kutekeleza miradi chini ya kiwango na kuongeza hasara kwa taifa.

HABARI KITAIFA

# TRA yaendelea kutoa elimu kwa walipakodi kukuza pato la taifa

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) mkoa wa kikodi Tegeta imesema itaendelea kutoa elimu kwa walipakodi na wafanyabiashara ili waone umuhimu wa kulipa kodi hiyo kwa hiari, hivyo kukuza pato la nchi.

Msaidizi wa Ukaguzi na Uhiari wa Ulipaji Kodi, Maigloria Saria, aliyasema hayo juzi baada ya kuwatembelea walipakodi eneo la Goba, Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam.

Alisema mamlaka hiyo inaendelea kusogeza huduma hizo kwa wafanyabiashara wa mkoa huo ili kuwarahisishia na kuepuka kupoteza muda mwingi kusafiri hadi makao makuu.

"TRA katika kampeni yetu ya mwezi huu wa Desemba tumelenga kuendelea kutoa elimu na kurudisha asante kwa walipakodi wetu, kuwasikiliza na kuchukua maoni yao katika kuelekea mwaka mwingine hasa katika ukusanyaji mapato ya serikali ili kulipa kodi bila usumbufu," alisema Maigloria.

Mkurugenzi wa Kampuni ya GAF International Group Limited, Flora Erasto alipongeza serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara na kushukuru TRA kwa kutambua kampuni yao kama walipakodi waaminifu na kuahidi kuendelea kufanya vizuri katika eneo hilo la kulipa kodi kwa serikali.

Flora alisema wataendelea kuwa waaminifu katika kutekeleza yale yote ambayo wanatakiwa kufanya katika biashara zao kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

Mfanyakazi wa kampuni ya B&B Specialized Polyclinic, Dk. Bhavin Jani alisema wako tayari kuendelea kuiunga mkono serikali kwa kulipa kodi kwa uaminifu na kwa kufuata taratibu na sheria zinazosimamia shughuli za biashara.

"Tunashukuru sana kwa kuthaminiwa na mamlaka zinazosimamia biashara kwenye nchi yetu, tunaahidi tutaendelea kufanya kazi kwa pamoja ili nchi yetu isonge mbele na maendeleo yapatikane," alisema Dk. Jani.

Alipongeza kitengo cha huduma kwa wateja cha TRA kwa kuongeza ufanisi katika utatuzi wa changamoto za wateja hasa katika kipindi hiki cha mabadiliko ya teknolojia.

"Ninaendelea kupongeza TRA kwa kuendelea kuboresha mifumo mbalimbali ya kodi licha ya kuwa hazijaisha zote, mfano ukilipa kodi, mfumo unaweza usikutambue kama umelipa kodi lakini hiyo haikufanyi ukashindwa kulipa na unapotoa taarifa kuhusu hilo watu wa huduma kwa wateja wanatatua kwa wakati," alisema Dk. Jani.



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza katika kikao kifupi na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mapato ya Oman, Nasser Khamis Al-Jashmir, kuhusu namna ya kuimarisha ushirikiano kati ya Oman na Tanzania katika eneo la kodi ili kurahisisha ufanyaji biashara kwa faida ya nchi hizo mbili. Waziri yuko katika ziara ya kikazi Muscat, Oman. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# 'Vyama upinzani ni vigumu kushika dola, vimevurugwa'

**Na Mussa Mwangoka,** KATAVI

KADA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Mbunge mstaafu wa Jimbo la Mpanda Mjini, Said Amour Arfi, amesema kwa sasa ni vigumu kwa Watanzania kuviamini vyama vya siasa vya upinzani na kuvipa dhamana ya kuongoza nchini kwa kuwa vimevurugwa.

Alivitaka lazima vijipange vizuri na vianze tena upya, japokuwa bado vina nafasi ya kukua na kuchukua na kuleta fikra zao mbadala kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii.

Alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake mjini Mpanda, alipotoa maoni yake kuhusu Watanzania kuviamini vyama vya upinzani na kuvipa dola.

Alfi ambaye aliwahi kuwa makamu mwenyekiti wa CHADEMA Taifa na Mbunge wa Jimbo la Mpanda kwa miaka 10 mfululizo kupitia chama hivyo kabla ya kukihama na kurejea CCM.

Alisema kwa mtizamo wake kwa sasa vyama vya upinzani havina nafasi ya kuaminiwa na wananchi katika nafasi ya kuongoza nchi, lakini vina nafasi ya kushiriki kwenye maendeleo ya nchi kwa maana ya kuwa na wawakilishi katika vyombo vya maamuzi, kama vitaondolewa kabisa ni kutowatendea haki wananchi.

**Alivitaka lazima vijipange vizuri na vianze tena upya, japokuwa bado vina nafasi ya kukua na kuchukua na kuleta fikra zao mbadala kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii.**

Akizungumzia kuhusu uchaguzi ujao wa madiwani, wabunge na Rais, alisema Tume Huru ya uchaguzi inapaswa kutenda haki kwa maana ya michakato yote iwe ya wazi, pia ione uwezekano wa kuvisaidia rasilimali fedha vyama vyote vya siasa ili kuondoa sintofahamu ya baadhi yao kushindwa kushiriki kikamilifu uchaguzi.

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Magharibi, Masanja Katambi, alisema anaona huo ndio muda mwafaka wa upinzani kushika dola kwa kuwa tangu kuingia kwa mfumo wa vyama vingi nchini wamepata uzoefu.

Alikiri kwamba serikali ya awamu iliyopita ilikandamiza upinzani, lakini hiyo haiondoi utayari wa wao kuchaguliwa na kuongoza dola kwa kuwa uundwaji wa serikali una wigo mpana na si kuangalia kundi dogo linalowazunguka.

KABWELA FADHILI MOHAMED



# Ummy: Utafiti muhimu kubaini matatizo ya wenye ulemavu

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, ameshauri kutolewa kipaumbele kwenye maeneo ya utafiti ili kubaini changamoto mbalimbali za watu wenye ulemavu.

Pia, alisema kuwa rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, imetoa msisitizo wa kuwekeza kwenye utafiti na kutumia matukio ya utafiti katika kuandaa sera na kufanya uamuzi katika sekta na ngazi mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Waziri Ummy aliyaeleza hayo juzi mkoani Dar es Salaam katika mkutano wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) na Tume ya Mipango uliokuwa unalenga kuhakiki Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, pamoja na kutoa maoni yatakayojumuishwa katika dira hiyo.

Alisisitiza kufanyika uamuzi katika kutengeneza sera, sheria na miongozo ambayo itasaidia kupeleka mbele kundi la wenye ulemavu nchini.

Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Mipango na Mwenyekiti wa timu kuu ya kitaalamu ya uandishi wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Balozi Dk. Asha Migiro, alisema rasimu ya dira hiyo imejikita katika misingi ya utawala, amani, usalama, na utulivu, huku ikiwajumuisha watu wenye ulemavu kwa namna ya kipekee.

Alisema kuwa msingi wa dira hiyo umejengwa juu ya nguzo tatu ambazo ni kujenga taifa jumuishi lenye ustawi, haki, na linalojitegemea, kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya jamii, na kujenga uchumi imara, jumuishi, na shindani.

"Katika nguzo ya pili, kipengele cha tatu kimetoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu kwa kuweka mkazo katika hifadhi ya jamii jumuishi. Pia eneo hilo linalenga kuhakikisha upatikanaji wa bima ya afya kwa wote, kutoa ulinzi dhidi ya uonevu na unyanyasaji, hususani kwa watoto, wanawake, na watu wenye ulemavu," alisema Balozi Migiro.

Alisisitiza kuwa uhakiki wa rasimu hiyo unalenga kubaini upungufu na kuyarekebisha, sambamba na kuongeza ambayo hayajajumuishwa. Na kwamba hatua hiyo inalenga kuhakikisha kuwa makundi yote, hususani watu wenye ulemavu, wanajumuishwa ipasavyo katika mipango ya maendeleo.

**MAONI**

Wakitoa maoni yao miongoni mwa wenye ulemavu, Francis Daula, kutoka Chama cha Wasiiona Tanzania (TLB), alitoa wito wa kushushwa kwa bei ya nishati safi na kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata matibabu ya uhakika bila vikwazo kufikia mwaka 2050.

Alisema licha ya kuainishwa kwa nishati safi kama sehemu ya masuala ya mazingira aliyoitaja kuwa ni hatua nzuri, lakini alidai kuwa changamoto ya bei ya juu bado inakwamisha upatikanaji wa nishati kwa watu wa vijijini na wenye kipato cha chini.

"Kama nishati safi tunataka tuitumie, basi kwenye dira iwekwe kipengele cha kushusha bei. Tuhamasishe matumizi yake, lakini pia bei ishushwe zaidi kwasababu nishati hiyo ipo nchini kwetu," alisema Daula.

Alisisitiza umuhimu wa Dira ya Maendeleo 2050 kuweka kipaumbele kwenye afya ya watu wenye ulemavu, akipendekeza kwamba kufikia 2050, mtu mwenye ulemavu awe na uhakika wa kupokea matibabu ya bure kwa asilimia 100, hasa kwa magonjwa makubwa.

"Sasa hivi tunaona madaktari bure, lakini dawa bado ni changamoto katika hospitali za serikali, hasa kwa magonjwa makubwa," aliongeza Daula, akieleza kuwa gharama za matibabu bado ni mzigo kwa watu wenye ulemavu, jambo ambalo linahitaji suluhisho la kudumu kupitia sera na mikakati madhubuti.

Naye Rehema Ibrahim alipongeza juhudi za serikali katika kuweka teknolojia saidizi kwa watu wenye ulemavu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), licha ya kuonesha wasiwasi kuhusu changamoto zinazowakumba watu wenye ulemavu katika vyuo vingine nchini.

"Nishauri kuwa rasimu ya Dira ya Maendeleo 2050 ionyeshe wazi mpango wa kuhakikisha vyuo vikuu vingine vikubwa vya serikali vinawekewa teknolojia saidizi ambazo zinaendana na wakati. Uwekezaji katika teknolojia hizi ni muhimu ili kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika masomo yao na kufikia malengo yao ya kielimu," alishauri Rehema.


CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30831 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

QUEEN ARNOLD MUSHI ................ ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: Queen Arnold Mushi of Plot No. P24009, Ada Estate Area, Kinondoni Municipality, DSM City

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the 19 day of December 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 23 day of November 2024

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

218295802

CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30817 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

KIZOTA AGRO PRODUCTS (T) LTD ....... ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: Managing Director, Kizota Agro Products (T) Limited of Plot No. 102, Uganda Avenue, Msasani Area, Kinondoni Municipality, DSM City

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the 19 day of December 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 23 day of November 2024

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

218295802

CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30824 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

LITTLE AGRET INVESTMENT CO. LTD ............ ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: Managing Director, Little Agret Investment Co. Limited of Plot No. P22221 Block B, Kisarawe II Area, Kigamboni Municipality, DSM

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the 19 day of December 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 28 day of November 2024

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

218295802

CR FORM NO. 7

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF KIVUKONI
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO: 30833 OF 2024.

THE REPUBLIC

*VERSUS*

GLADSON NAFTAL URIO ...................... ACCUSED PERSON

Summons to an Accused Person
*(Sections 130 and 100 of the Criminal Procedure Act)*

To: Gladson Naftal Urio of Plot No. 1844, Block A, Buguruni Area, Ilala Municipality, DSM

WHEREAS your attendance is necessary to answer a charge of Engaging unregistered person or firm Contrary to Section 22(4) of the Contractors Registration Act Cap. 235 of the Laws, you are hereby required to appear in person before this Court on the 19 day of December 2024

Herein fail not.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 23 day of November 2024

Resident Magistrate
RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

218295802



# Machifu wavunja ukimya matambiko funga mwaka

**Na Mary Mosha,** HAI

BAADHI ya viongozi wa mila mkoani Kilimanjaro wamevunja ukimya wakisema ujio wa wachaga wakati wa sikukuu kutoka ndani na nje ya nchi ni kuenzi mila njema kwa kukutana baada ya muda mrefu wa utafutaji mali.

Wakizungumza katika hafla ya kumsimka Chifu wa Machame anayesimamia koo 52, Gilbert Shangali, Mchili George Kavishe kutoka Rombo, alisema kuwa dhana ya kufanya matambiko wakati huo hususani wa sherehe za mwishoni mwa mwaka za Krismas na Mwaka Mpya si sahihi katika jamii hiyo ya Wachaga.

"Watu wengi huja kwa ajili ya kukaa pamoja, kuzungumza, kukosoana na kufanya tathimini ya yale waliyoyafanya kwa kipindi cha mwaka mzima.

Katika kukutana na wapendwa wao yapo mambo mengi yanayofanyika kama ishara njema na upendo," alisema Kavishe.

Aliyataja mambo hayo kuwa ni pamoja na kufanya ibada za familia, usafi kwenye makaburi, kutatua migogoro.

Alisema mambo hayo yanaleta tija katika ukoo husika kwani kuna nyakati wanapendezeka maendeleo, kuoa, kuacha tabia mbaya na kuzidisha ushirikiano.

"Wapo wachache kwenye jamii ambao wanakaidi kutokana na tabia hizo kuota mizizi ila tunahakikisha tumewachukulia hatua kwa kushirikiana serikali, wale wote wanaoshindwa kuja nyakati za sikukuu za mwisho wa mwaka, sisi tunawahesabu kama wavivu na wasiojituma, hivyo serikali iwachukulie hatua," alisema Mchili Laurence Mlay kutoka Mwika.

Baadhi ya wananchi, akiwamo Elisaria Mbowe, alisema kwenda katika sherehe za mwisho wa mwaka ni ishara ya upendo kwa familia na kuiomba serikali kuruhusu kuwa sheria.

Mbowe, alisema kuna watoto hutelekeza familia zao, wazazi na ndugu na jamaa zao na kutaja kuwa ni laana kwenye jamii.

"Kuwatumia wazazi wako pesa na kuwapigia simu kwa kipindi cha mwaka mzima sio sawa, ni wajibu wa kila mtu kwenda nyumbani kwao hasa nyakati za mwisho wa mwaka ili kupata baraka za wazazi, viongozi wa dini na jamiii," alisema Wilson Lema.

Kwa upande wao, wanawake wa jamii ya wamachame, akiwamo Suzana Lema, walimwomba Chifu aliyesimikwa kudhibiti vijana wanaokunywa pombe kupita kiasi, wavivu, wanaotumia dawa za kulevya na kushiriki vitendo vya ulawiti na ushoga katika jamii.

"Wengine tunakufa bila kupata wajukuu, kizazi chetu kitapotea, vijana wa kike na wa kiume hawataki kutimiza majukumu yao, hii sio sawa.

Mangi tusaidie wapate watoto tena wenye maadili ya jamii zetu," alisema Florence Nkya.

Akisoma risala ya kiongozi wa machidu Mkoa wa Kilimanjaro, Mangi Mariale alimtaka chifu huyo kuhakikisha anasimamia haki, umoja, mshikamano na kutatua migogoro ya ardhi.

"Sitegemei kusikia migogoro ya ardhi, kuwaona vijana wanatumia dawa za kulevya na kunywa pombe kupitiliza na kusahau majukumu ya kutunza familia," alisema Mariale.

Askofu Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Fredrick Shoo, alimtaka kiongozi huyo kusimamia maadili na mila njema katika jamii na kuwa mfano wa kuigwa kusimamia upatikanaji haki.

"Tunatambua babu yako alikuwa kiongozi wa kimila na ndiye aliyeweza kuwapokea Wamisioni wa kwanza huku Machame na baadaye alibatizwa, hii ni kusema alikuwa na hofu ya Mungu na alimpenda Mungu, Tunaomba uige kwa kuwa kiongozi bora mwenye kutenda yaliyo mema na yanayoleta mabadiliko katika jamii zetu, " alisema Dk. Shoo.




Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM, Wilaya ya Babati Mjini, Mkoani Manyara, Emmanuel Khambay, akizungumza kwenye mahafali ya Chuo cha Uhasibu baada ya kuhitimu shahada ya uzamili ya utawala, biashara, uongozi na uwajibikaji, jijini Arusha juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## RC akunwa miradi kuajiri vijana

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Balozi Batilida Buriani, ameeleza kufurahishwa na miradi ya Tanga Yetu kujikita kutatua tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana jijini hapo.

Balozi Batilida, alitoa kauli hiyo wiki iliyopita wakati akizindua Mradi wa GOYN na Jukwaa la Vijana Tanga.

Alisema amefurahishwa na jinsi mradi huo ulivyowezesha vijana katika jiji hilo kuondokana na tatizo la ukosefu wa ajira na kujikwamua kiuchumi.

"Kama tunavyoona uwepo wa majukwaa na viongozi ambao wanatambulika na jiji. Niwapongeze kwa mashirikiano haya na naamini Tanga Yetu inaenda kuwa ni mahali pazuri kwa ustawi wa watoto na vijana," alisema na kuisisitiza kuwa:" Sisi kama serikali ya Mkoa, tunaahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kuandaa mazingira rafiki kwa wawekezaji pasipo kuwa na urasimu wowote."

Mkuu huyo wa mkoa, alitoa wito kwa uongozi wa jiji hilo kuwapa ushirikiano wadau wa maendeleo na kusimamia miradi kwa lengo la kuboresha ustawi wa vijana katika maeneo yao.

Vilevile, alitoa wito kwa vijana kutumia fursa hiyo adimu kushiriki katika miradi hiyo, kujituma katika utekelezaji wa yale wanaojifunza na kuyafanya yawe endelevu kwa manufaa yao na vizazi vijavyo.

"Naomba sana wananchi wenzangu na wadau wengine wote tushirikiane ili jambo hili lifanikiwe zaidi na kuwa endelevu," alisema.

Kwa upande wa Halmashauri ya Jiji hilo, alilitaka kuendelea kushirikiana na Program ya Tanga Yetu na wadau wengine kuhakikisha wanaandaa Jukwaa kama hili kama mwaka kama ilivyoazimiwa ili kuonyesha matokeo ya maendeleo ya vijana.

Uzinduzi huo uliambatana na wa kongamano ambalo pamoja na mambo menine, mada mbalimbali zilijadiliwa ikiwemo ujuzi, upatkanaji wa mitaji kwa vijana, fikra na mtazamo wa vijana kujiajiri na kuajiriwa.

# Wasichana wajifungua watoto mijini, wawatelekeza vijijini

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

BAADHI ya wasichana wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro wametakiwa kuacha tabia ya kuzaa watoto mjini na kuwatelekeza kwa wazazi wao vijijini na kukua katika mazingira magumu na hatarishi.

Rai hiyo imetolewa na Diwani wa Kata ya Masama Magharibi, Mashoya Natai, wakati wa sherehe ya kukabidhi misaada kwa watoto yatima na wanaoishi mazingira magumu wa Kituo cha Lukani.

Natai ambaye ni kiongozi wa kituo hicho, alisema kitendo cha wasichana hao kuwatelekeza watoto hao kwa wazazi wao na kurejea mjini kinasababisha kuwa na malezi yasiyofaa na kuchangia kuendelea kukithiri kwa mmomonyoko wa maadili katika jamii.

Ameomba wasichana hao kuzaa kwa kufuata utaratibu baada ya kuwa na uwezo wa kuwalea watoto wao badala ya kuwatwisha mzigo wazazi wao na kusababisha kushindwa kushiriki kikamilifu katika miradi ya maendeleo ya kuwaingizia kipato na kukithiri kwa umaskini.

Natai, alisema kwenye vituo vya watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu, wengi wao ni watoto waliotelekezwa na wazazi wao na kukimbia mjini kwa kisingizio cha kutafuta maisha.

"Wito wangu kwa hao wanaowatelekezea wazazi watoto wao, kama kweli maisha uko mjini yamekuwa magumu, wanapowaleta basi angalau wawasapoti wazazi kwa chochote kitu," alisema.

"Kuwatumia kitu kidogo kuwasapoti watoto wao ni jambo la kiungwana kabisa, lakini wanawaachia kabisa wazazi bila kutumia kitu chochote ili jambo sio sawa, japo watakuwa vitu vingi wanavikosa katika maisha yao," alisema.

Alisema wazazi wengine ni wazee na kwamba wamechoka hawana chochote bado wanawaongezea mzigo wa kulea watoto.

"Tufuate utaratibu wa kupata hawa watoto na kuwatunza sisi wenyewe, kwani inakuwa rahisi kuwaepusha na madhila mbalimbali ikiwamo vitendo vya ukatili dhidi yao," alisema diwani huyo.


Mchungaji Thomas Kudalisamu wa Dayosisi ya Kaskazini Jimbo la Hai Usharika wa Ng'uni, alisema kuna haja serikali, kanisa na jamii kuungana kupinga tabia hiyo ili watoto wapatikane kwa utaratibu unaotakiwa na malezi bora.

"Ni kweli wapo kina dada ambao wanapata watoto, na watoto wale wakati mwingine wanawapata wakiwa mjini, wanapojifungua wanawaleta kwa wazazi vijijini na kuwa mzigo kwa kulea vile vichanga na wale ni babu na bibi nguvu zimepungua," alisema.

Alisema watoto hao katika kukua kwake hakuna wa kumuonya na kumwelekeza na kuwa na maadili mabaya.

Awali katika taarifa yake, Mwalimu Esther Liyamuya, aliiomba serikali kuwaunga kwa kutoa misaada ya kijamii kwa ajili ya kuwasaidia watoto hao.

Aliwashukuru marafiki wanaojitolea kutoa misaada kwa watoto hao ili kuhakikisha wanapata mahitaji muhimu kwa kuwa ni sehemu ya jamii.





# Upandaji miti washika kasi Buchosa

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

ZAIDI ya miti 2,000 imepandwa katika Shule ya Msingi Lumea iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, ukame na ongezeko la joto.

Akizungumza wakati wa upandaji miti hiyo, Muhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) Wilaya ya Sengerema, Stephen Oyugi, alisema jamii inatakiwa kuongeza juhudi kupanda na kuhifadhi miti ili kuiweka Tanzania salama.

Oyugi, alisema katika kukabiliana na ongezeko la ukame na joto katika wilaya hiyo, TFS wametoa bure miche zaidi ya 37,000 kwa kipindi cha robo ya mwisho ya mwaka na kuendelea kuotesha mingine.

Alisema kampeni hiyo ni endelevu ili kulinda na kutunza mazingira na kwamba watahakikisha miti yote iliyopandwa inastawi.

"Miti inahitaji kumwagiliwa maji, kupunguzaji matawi mara moja kwa mwaka badala ya mara kwa mara kama ambavyo wengi wanavyofanya kwani ni kumaliza vyanzo vya chakula kwa mti huo," alisema Oyugi.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Msaghaa Hango, alisema kampeni hiyo ni utekelezaji wa lengo la kupanda miti 6,000 na kuahidi kuendelea kuongoza mingine na kutoa elimu kwa wanafunzi ya utunzaji.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Sengerema, Cuthbert Mdala, alisema upandaji miti ni kipaumbele cha Sengerema na imekua ikifanya vizuri kufikia lengo la kitaifa la kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka.

**Alisema kampeni hiyo ni endelevu ili kulinda na kutunza mazingira na kwamba watahakikisha miti yote iliyopandwa inastawi.**

# Wenyeviti CHADEMA wabwaga manyanga, watimkia CCM

**Na Samson Chacha,** TARIME

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wilayani hapa Mkoa wa Mara kimepata pigo baada ya wenyeviti wake watatu vijiji na vitongoji kujiuzulu na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa madai ya kuwaletea maendeleo wananchi.

Wenyeviti hao wamedai kuwa wamechukua uamuzi huo kutokana na kukosa kuungwa mkono na wajumbe ambao sehemu ni wa CCM.

Wenyeviti hao ni wa Kijiji cha Nyabisaga, Sagamo Nyamangondi, Kitongoji cha Kegesambi, Chacha Mogore na Kitongoji cha Nyairoma, Masha Vicent.

Wenyeviti hao walitangaza uamuzi wao huo juzi wakati wa sherehe ya CCM kuwapongeza wenyeviti wa vijiji na vitongoji wa chama hicho waliochaguliwa katika uchaguzi uliofanyika Novemba 27, mwaka huu.

Wakizungumza katika sherehe hizo zilizofanyika katika Uwanja wa Tarafa ya Sirari, wakiongozwa na Sagamo Nyamangondi, walisema mbali na kushinda nafasi hizo, kutokana na wajumbe karibu wote kuwa wa CCM itakuwa vigumu wao kufanya kazi ya kuwaletea maendeleo wananchi peke yao.

**Wenyeviti hao ni wa Kijiji cha Nyabisaga, Sagamo Nyamangondi, Kitongoji cha Kegesambi, Chacha Mogore na Kitongoji cha Nyairoma, Masha Vicent.**

"Kwa kuwa nia yetu kuwaletea wananchi waendeleo tumeamua kujiuzulu uongozi na kujiunga na CCM ili kuungana na wenyeviti waliopita na wajumbe kuleta maendeleo kwa wananchi wetu," alisema Nyamangondi.

Katibu wa CCM Wilaya ya Tarime, Noverty Malima, aliwapongeza wenyeviti hao kwa uamuzi wao na kuahidi kuwapa ushirikiano kujenga Tarime na Taifa na kuwaletea wananchi maendeleo.

Diwani wa Kata ya Sirari, Amos Sagara, alisema mji huo una wakazi wengi na kuendelea kukua kwa kasi, hivyo wanahitaji juhudi za viongozi kuleta maendeleo na sio kubaki kwenye siasa zisizo na tija.

Alisema wamepeleka maombi ya kupatiwa Mamlaka ya Mji ili kuongezea hadhi mji huo na kuwa mamlaka.

"Tunaomba serikali iweze kusikiliza maombi yetu ya siku nyingi tangu wakati wa uongozi wa awamu ya nne," alisema Sagara.

Kutokana na uamuzi wa wenyeviti hao wa CHADEMA katika Halmashauri ya Tarime Vijijini kimebaki na wenyeviti wa vijiji watatu na vitongoji 30 huku CCM kikiwa na wenyeviti vijiji 84 na vitongoji 468.



Mkurugenzi wa Shirika la Akili Platform Tanzania (APT), Robert Roght (kulia), akiwa na wanachama wenzake wakichukua miche ya miti mbalimbali kwa ajili ya kupanda katika eneo la kituo cha watoto cha Huruma Vision Tanzania kilichopo Urambo, Tabora kama ishara ya kufunga mwaka 2024 juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia ang'ara tuzo ya utawala bora

**Na Vitus Audax,** SENGEREMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametunikiwa tuzo maalum ya utawala bora nchini na kuleta maendeleo katika kipindi kifupi cha uongozi wake.

Samia ni miongoni mwa watu zaidi ya 30 waliotunikiwa tuzo kutoka sekta mbalimbali katika awamu ya nne ya Usiku wa Tuzo za Kanda ya Ziwa chini ya usimamizi wa Kampuni ya Eagle Entertainment.

Akikabidhi tuzo hiyo kwa Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda wilayani Sengerema, Mwandaaji, Hassan Kuku, alisema inalenga kutambua mchango Rai Samia kuongoza Taifa na kutekeleza miradi kwa muda mfupi.

"Hii tuzo tunaitoa kwa sababu ya uthubutu alioonyesha rais wetu Samia Suluhu Hassan kusimamia shughuli za serikali, tunajua wengi hasa ambao tumeathiriwa na mfumo dume tulikuwa tukijiuliza je, tutafika katika hii safari ambayo aliachiwa na mtangulizi wake, John Pombe Magufuli," alisema Kuku.

Alisema kwa uwezo wa Mungu, Rais Samia amesimamia shughuli zote za serikali ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi mbalimbali iliyoachwa na mtangulizi wake bila kuteteleka, hivyo anastahili tuzo ili imwongezee nguvu katika utendaji wake.

Aliiomba serikali kuwezesha utoaji wa tuzo nyingine Kanda ya Ziwa ili kusaidia kuwatambua watu wenye michango ya kimbadiliko katika jamii.

Kuku, alisema bado wanahitaji uwezeshwaji wa kutoa tuzo kutoka sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na sanaa na muziki, utawala, michezo, habari na mawasiliano.

Alisema uandaaji wa tuzo hizo umekuwa ukihitaji uwekezaji mkubwa kusaidia kuinua washindi.

Akipokea tuzo hiyo kwa niaba ya Rais Samia, Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake, miradi ya maendeleo imeendelea kutekelezwa na kuvutia uwekezaji kwa mkoa na wilaya hiyo.

"Miradi ni mingi kwa sasa zikiwamo barabara pamoja na daraja kubwa ya J.P.Magufuli ambalo lipo katika hatua za mwisho kukamilika kwake, imevutia uwekezaji ikiwemo uanzishwaji wa mgodi wa dhahabu Nyanzaga unaotaraijiwa kuanza hivi karibuni," alisema Ngaga.

Katika usiku wa tuzo zaidi ya washindi 30 kutoka sekta mbalimbali walitunukiwa tuzo hizo.

Kwa upande wa waandishi wa habari kutoka Kampuni ya The Guardian ltd Vitus Audax na Neema Emmanuel waliibuka washindi wa pili na watatu vipengele vya uandishi bora wa habari za mazingira na unyanyasaji wa kijinsia.


Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 17, 2024
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI


Ukurasa 14

**Wanaolia Januari ni chungu, kumbukeni nidhamu ya pesa**


Ukurasa 12

Asasi yawagusa waraibu 1,000 wajitambua, kufahamu haki zao


Ukurasa 13

MAAJABU NYANGUMI DUME

NA MWANDISHI WETU

# Vitambue vyanzo vya ajali ili uzikwepe

## • Saidia majeruhi si kupora, kuua

UMOJA wa Mataifa (UN), unazitaja ajali za barabarani kuwa ndizo zinazoongoza kuua vijana Afrika.

Ni tangazo la Mei mwaka jana, linalozitaja serikali za Afrika zichukue hatua mpya za pamoja kuzikabili, taarifa hizi zinawafikia wananchi wakati wa Wiki ya Kimataifa ya Usalama Barabarani, inayoadhimishwa Mei 15 hadi 21kila mwaka.

Ajali ni kitisho cha maisha kwa Watanzania mfano mabasi ya A-N Classic likitokea Mbeya kwenda Tabora liliua 12 na kujeruhi zaidi ya 30 wakati Asante Rabi lililosababisha vifo vya watu wanane na kujeruhi 39 mkoani Mwanza.

Kutokana na ajali hasa kuelekea wakati huu mwisho wa mwaka ni lazima kila mmoja kujilinda, kujiepusha na kusaidia wanaopata ajali.

Ajali au dharura zinaweza kusababisha majeraha na maumivu, ulemavu, vifo na uharibifu wa mali na hivyo kuleta umaskini kwa watu na taifa.

Ili kuziepuka ni vyema kukumbushana suala la kutii sheria za usalama barabarani maana ndiyo mwongozo.

La kwanza madereva kumbukeni upande unaotakiwa kukaa wakati wa kuendeshea. Angalia wakati gani taa zinaruhusu au kukataza kuvuka na kuheshimu maelekezo.

Mambo yasiishe hapo ni vyema kukumbuka kuheshimu vivuko vya watembea na kuwajali wenye ulemavu, watoto wadogo na wazee.

Jingine ni kuacha kuendesha magari mabovu, kuepuka kuendesha gari ukiwa umelewa na kama umepanga kunywa kodi gari au omba dereva mwingine wa kukuendesha.



Ajali zinaweza kuepukwa na kuzuiliwa kwa kuwa makini zaidi. **PICHA: MTANDAO**

Acha kuendesha gari kwa kasi wala kwa mwendo mdogo fuata maelekezo ya kasi 'speed' yanayoonyeshwa kwenye barabara.

Jambo muhimu ni kufunga mkanda kila wakati unapokuwa kwenye gari.

Ni jambo la kuzingatia, kadhalika mlinde mtoto kwenye kiti chake na kumfunga mkanda.

Kama unaendesha pikipiki vaa kofia ngumu dereva na abiria wake. Aidha ni vyema kuzima simu na usiendeshe gari au pikipiki ukiwa unachati, unatuma ujumbe au kusikiliza muziki ukiwa na foni masikioni.

Uoni hafifu ni kisababishi cha ajali kwa hivyo kwa kuzingatia jukumu la dereva kuepusha hatari pima macho kila unapohitaji leseni au kila wakati kuhakikisha uzima wake kwa kuwa wewe ni dereva.

**KUSAIDIA MAJERUHI**

Kwa ujumla ajali zipo na pengine haziepukiki ili kusaidia majeruhi ni muhimu na cha kwanza kuangalia ni uhai wa mtu unayemwokoa pamoja na uzima wako.

Hivyo ni muhimu kuchukua tahadhari usigusane na damu za majeruhi kuepusha kuambukizwa maradhi. Kingine muhimu ni kujua kuwa majeruhi hufariki kutokana na kutokwa na damu nyingi pamoja na kukosa hewa safi baada ya kubanwa au kuumizwa mfumo wa hewa.

Ikumbukwe kuwa ubongo wa binadamu hauwezi kuishi bila hewa safi ya oksjeni kwa dakika sita baada ya hapo hufa.

Kwa hiyo kwa majeruhi yeyote ni lazima mfumo wa hewa ufuatiliwe na hasa namna ya kupumua kama inavyopasa na pia kumhakikishia mzunguko wa damu na kufahamu iwapo anajitambua au amepoteza fahamu.

Kikubwa kingine cha kuwaangalia majeraha ni iwapo njia ya hewa iko salama na mgonjwa anapumua na kama kuna sehemu inayotoka damu izuie.

Watu wasiwasonge na kuwazingira majeruhi, kaa mbali wapate hewa, fungua vifungo, tai, mikanda na kulegeza nguo zinazowabana.

Acheni kuwaibia majeruhi au kuwaia ili kupora mali. Ni jinai.

**KUZUIA AJALI**

Anza na epusha kunguka. Watoto ni kundi linaweza kuanguka chini wakati wote. Ni vyema wawe na waangalizi muda wote nyumbani na popote.

Kadhalika waangaliwe hata wakati wanapocheza wawe salama na vifaa wanavyotumia viwe salama pia.

Kama ni ndani ya nyumba waangaliwe wasicheze kwenye sakafu yenye maji watateleza. Kuwe na mwanga wa kutosha. Wasioona wawe na waangalizi.

**KUACHA UGOMVI**

Mambo yanayosababisha ugomvi ni mengi lakini mojawapo ni ulevi epuka. Achana na kutumia dawa za kulevya, pombe na bangi kwani vinachangia ugomvi.

Lakini pia si vyema kujichukulia maamuzi ya kuwaadhibu wengine, watu waache kujichukulia sheria mkononi kwa kuwaadhibu watuhumiwa wa makosa mbalimbali.

**HADHARI YA MOTO**

Moto unaweza kusababisha hatari hivyo watoto wasiachwe bila uangalizi kwani ni rahisi kuangukia maji yanayochemka, vyakula hasa chai au uji na moto wenyewe.

Kwa wenye kifafa, wagonjwa na wazee ni lazima waepushwe na ajali na kuwapa wasaidizi tena wasikae karibu na moto na maji ya moto.

Wakati mwingine umeme nao ni chanzo cha ajali watu wajali na kuzingatia masuala ya usalama na kutumia vifaa vya umeme kwa usahihi.

Mfano, ukimaliza kupasi ichomoe kwenye moto, kuzuia ajali kwenye mifumo ya nyumbani.

Ulevi kupindukia ni jambo linaloweza kusababisha ajali ya moto, mfano kuwasha jiko ili kupasha

INAENDELEA UK. 12

ELIMU

**NA SABATO KASIKA, BAGAMOYO**

# Asasi yawagusa waraibu 1,000 wajitambua, kufahamu haki zao

WARAIBU 935 wa dawa za kulevya wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, wamefikiwa na elimu ya kujitambua baadhi wakiachana na dawa huku wakifahamu na kudai haki zao za msingi za kibinadamu .

Ni katika kipindi cha mwaka mmoja wa 2024, ikianza kutolewa mwanzoni mwa mwaka huu na shirika la kuhudumia waraibu la Life & Hope Rehabilitation Organisation (LHRO) katika kata tano wilayani humo.

Haki wanazostahili ni kupata bure methadone dawa za kuulazimisha mwili kuachana uraibu wa dawa za kulevya kutoka vituo na hospitali za umma.

Hayo yamo katika taarifa ya hitimisho la mradi wa utoaji elimu iliotolewa na Mkurugenzi wa Shirika hilo, Al-karim Bhanji mbele ya wadau wanaohudhuria mkutano wa kuhitimisha mradi huo mjini Bagamoyo hivi karibuni.

Kingine ni kuthaminiwa katika jamii na kupewa huduma muhimu za afya, elimu upendo.

"Ndani ya mwaka huu mradi umefikia waraibu 935, wa kike 29 ambao wote tumewapa elimu ya kujua haki zao za msingi katika kata za Dunda, Magomeni, Kisutu, Nianjema na Kiromo," anasema Bhanji.

Anasema LHRO ilipanga kufikia waraibu 800 lakini ikavuka, kwa maelezo kwamba fedha za mradi kutoka kwa wafadhili zilifika kwa wakati, walipata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa watumishi wa serikali na pia uboreshaji wa mafunzo kwa watoa elimurika.

Anasema elimu waliotoa imesaidia waraibu 422 kubadili tabia na kuanza kutumia dawa ya methadone, wa kike wakiwa 11 na wengine 513 wakiwa bado hawajafikia uamuzi wa kuanza dozi ya methadone.

Bhanji anasema suala la kuamua kuacha dawa hizo, linategemea utayari wa mhusika na kwamba



Mkurugenzi wa LHRO, Al-karim Bhanji, akitoa taarifa katika mkutano wa wadau. Kulia ni Kaimu Mkuu wa Kituo cha Polisi Bagamoyo, Tumaini Mgobela na Mganga Mkuu wa wilaya, Dk. Kandi Lussingu (wa pili kushoto). **PICHA: SABATO KASIKA**

iwapo LHRO itapata fedha nyingine toka kwa wafadhili watarudi Bagamoyo kuendelea kutoa elimu ili kusaidia vijana kuacha dawa za kulevya na pia kupunguza unyanyapaa dhidi yao.

**UTEKELEZAJI**

Bhanji anasema ili kufikia malengo ya mradi, afua mbalimbali zilitekelezwa kupitia semina elekezi, elimu ya mtu mmoja mmoja, mikutano ya hadhara, kupitia vyombo vya habari, mahubiri ndani ya nyumba za ibada, ushirikishwaji wa waraibu na elimu kwa makundi rika.

Anasema wamefikisha elimu hiyo kwenye shule tisa zikiwamo tano za msingi, vijiwe 14 vya bodaboda, masoko manne, makanisa matatu, misikiti sita mahakama mbili, vituo viwili vya polisi na polisi kata wote wilayani Bagamoyo.

"Tulitoa elimu kwa polisi kata na dawati la jinsia wote wa wilayani Bagamoyo, tukijikita kwenye suala la unyanyapaa, kwa sababu walikuwa wakilaumiwa kukiuka haki za waraibu," anasema.

Anasema wamezifikia masikani 18 za waraibu na pia wametoa elimu kwa makundi mbalimbali ili yaunge mkono jitihada za kuokoa waraibu wa dawa za kulevya na pia kuondoa unyanyapaa dhidi ya kundi hilo.

"Wengine waliopata elimu ni watendaji wa kata, watumishi wa halmashauri ambao ni watekelezaji wa sera mbalimbali za afya na uchumi katika wilaya ya Bagamoyo," anasema.

Anafafanua kuwa shirika lilitoa fursa kwa vijana wawili kutoka kila kata yenye mradi ambao walikuwa wakipata huduma ya upataji nafuu na kuwajengea uwezo kuhusu namna ya kutekeleza mradi ili wasaidie waraibu kubadilika.

"Tunawashukuru Mfuko wa U.S. Ambassador Fund for HIV/AIDS Relief (AFHR Grant) and Pepfar kwa kufadhili mradi huu na wadau wengine ambao wamechangia kuufanikisha," anasema.

Anasema wadau hao wengine anaowataja kwa majina ya CDC, THPS wanaopambana na UKIMWI kwa ajili ya kuendeleza miradi ya MAT Clinic, kwamba wamechangia kufanikisha elimu hiyo.

"Lakini pia tuna ombi kwa serikali kwamba iendelee kuwatumia waelimishaji rika waliowezeshwa ili nao waendelee kuelimisha na kuibua na kufuatilia waraibu walio kwenye huduma za methadone na wanaotumia dawa za kufubaza VVU," anasema.

Anaongeza kusema; "Pamoja na hayo, shukrani zetu zifike kwa mkurugenzi wa halmashauri ya Bagamayo, ofisi ya mganga mkuu, ustawi wa jamii, watendaji wa vituo vya afya, ofisi ya mkuu wa polisi wilaya kwa kuwa nasi kila hatua ya utekelezaji wa mradi huu," anasema.

**USHAURI WA WADAU**

Mganga Mkuu wilaya hiyo, Dk. Kandi Lussingu, anawataka LHRO kuendelea kushirikiana na serikali kwa kubuni shughuli mbalimbali ambazo vijana walioacha dawa za kulevya wanaweza kuzifanya.

Dk. Kandi anasema vijana walioacha dawa hizo wakiendelea kuishi katika mazingira ya awali yaliyosababisha wakatumia dawa hizo, wanaweza kujikuta wakarudia uraibu.

"Hivyo, wito wangu kwenu LHRO, mjaribu kubuni hata miradi midogo ambayo wanaweza kuifanya na kujiingizia kipato, ninaamini serikali itawaunga mkono katika jambo hili," anasema Dk.Kandi.

Anaongeza kuwa ikiwezekana, waanzishe darasa kwa ajili ya kutoa elimu ya uzalendo kwa vijana hao kwa nchi yao na kuwafundisha nyimbo zinazohamasisha uzalendo.

"Mkifanya hivyo mtakuwa mmewasaidia, sisi kwa upande wetu tunaendelea kuwapokea na kuwapa dawa za methadone, lakini wadau kama nyie mwendelee kutusaidia kwa kubuni mbinu ambazo zitawawezesha kuwa raia wema," anasema.

Kaimu Mkuu wa Upelelezi wa wilaya hiyo, Veronica Salala, anawataka polisi kata wote kuwatambua vijana walioacha uraibu katika maeneo yao na kuweka mikakati ya kuhakikisha hawarudi kwenye vitendo hivyo.

"Mnaweza kuwa mnaonana nao kila mara na kuwahamasisha muhimu wa kufanya shughuli halali za kujipatia kipato badala ya kushinda vijiweni ambako ni hatari kwa maisha yao," anashauri Veronica.

# VITAMBUE VYANZO VYA AJALI ILI UZIKWEPE

**INATOKA UK.11**

chakula au kupika kisha kujisahau, kuwasha pasi na kujisahau, kuwasha sigara na kujisahau na kusababisha kuchoma godoro chumba, meza na viti sebuleni.

**UANGALIFU MAJINI**

Ajali hizi zinaepukwa kama huna ujuzi wa usalama wa maji usiingie majini. Kadhalika kama unakwenda ufukweni na watoto wasimamie wakati wote.

Wafuatilie na weke jicho lako kwa watoto wanapokuwa ndani au karibu na maji.

Usiruke ndani ya maji ili kuokoa mtu utazama kama huna uwezo. Ni vizuri kuweka uzio kuzunguka bwawa la kuogelea kunusuru watoto.

Kama umelewa acha kuogelea na pia mvua zinanyesha umelewa na unataka kuvuka mto au mkondo acha unaweza kuzama.

Aidha ukiwa na akili timamu ingiza fimbo kupima kina cha maji na si miguu, lakini kama kuna mvua kubwa na mafuriko usivuke mto na ikibidi kaa mbali na mifereji ya maji, mito na madimbwi.

**EPUKA WANYAMA**

Zipo ajali zinazoweza kutokea kutokana na wanyama mfano kwa wanaoishi vijijini au waliozungukwa na vichaka ni vyema kuwa waangalifu na wanyama kama nyoka na hata simba au chui.

Kwa wanaoogelea ni vyema pia kujikinga na mamba mtoni. Kumbuka kuepuka kuingia vichakani wakati wa jua, kadhalika kutembea peke yako nyakati za usiku.

***MITANDAO***

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# MAAJABU NYANGUMI DUME

## Alitoka Colombia akatua Zanzibar



TANZANIA ni moja ya nchi yenye vitu vingi vinavyoshangaza na wakati mwingine huchochea mijadala ambayo inazidi kuitangaza kiutalii na kuvutia watafiti na watalii.

Mfano wa maajabu ni kuhama kwa nyumbu kutoka mbuga ya Serengeti kuelekea nchi jirani ya Kenya kwenye hifadhi ya Maasai Mara wakati wa kupata mimba, lakini pia hurudi na kuzalia Serengeti.

Pamoja na hilo ipo hifadhi ya Ngorongoro Creter ambayo ni moja ya maajabu ya dunia ambayo ni makazi ya binadamu na wanyamapori, bila kuwa na matatizo.

Hivi karibuni kuna tukio ambalo limesababisha wanasayansi kuanza kufanya utafiti baada ya samaki mkubwa nyangumi kusafiri kwa umbali mrefu kutoka Bahari ya Pasifiki nchini Colombia hadi Tanzania akitua ndani ya Bahari ya Hindi.

Columbia iko bara la Amerika Kusini ambalo ni mbali mno kwa safari ya kiumbe huyo.

Nyangumi huyo mwenye nundu anadaiwa ndiye samaki wa aina hiyo aliyefanya uhamaji wenye masafa marefu zaidi na ya kipekee ambayo hayajawahi kurekodiwa.

Wanasayansi ambao wanachunguza safari hiyo ya nyangumi, wanaeleza huenda umechochewa na mabadiliko ya tabia nchi.

Nyangumi huyo alionekana katika Pasifiki karibu na Colombia mwaka 2017, kisha alikutwa tena miaka kadhaa katika Bahari ya Hindi kisiwani Zanzibar, umbali wa kilomita 13,000.

Katika utafiti uliochapishwa na jarida la sayansi, la Royal Society Open Science, wataalam wanaamini kuwa safari hiyo ndefu inaweza kuwa imesababishwa na mabadiliko ya tabia nchi.

Mabadiliko ya tabianchi yanachangia kupungua kwa hifadhi za chakula au safari ya kutafuta wenza.

Ekaterina Kalashnikova kutoka kwa programu ya mamalia wa baharini Tanzania, anasema kwamba tukio hilo ni la kushangaza na la kipekee hata kwa aina hiyo ya wanyama wanaohama.

> ''Ingawa sababu halisi bado hazijabainika, lakini uhamaji wa nyangumi wenye nundu huenda unachochewa na mabadiliko ya tabianchi, mazingira mabaya ambayo yanatokea kila wakati na mabadiliko ya spishi,'' anaongeza Dk. Kalashnikova.

Dk.Kalashnikova anasema kuwa kuna uwezekano kuwa umbali aliosafiri ni mrefu zaidi kuwahi kurekodiwa kwa nyangumi mwenye nundu.

Hata hivyo, aina hiyo ya nyangumi wenye nundu huishi katika bahari zote duniani.

Pia husafiri umbali mrefu kila mwaka na wanahama kwa umbali mrefu kuliko mamalia yoyote, wakisafiri kutoka maeneo ya kitropiki ambayo wanapozaliana maeneo yenye chakula katika maji baridi.

Lakini safari ya nyangumi huyo dume ilikuwa ya kipekee zaidi, ikiwa na maeneo mawili tofauti ya kuzaliana.

Nadharia moja ni kwamba mabadiliko ya tabia nchi yanabadilisha wingi wa uduvi kamba wadogo wanaoliwa na nyangumi hivyo kuwalazimu kuhamia bahari tofauti kutafuta chakula hicho.

''Ingawa sababu halisi bado hazijabainika, lakini uhamaji wa nyangumi wenye nundu huenda unachochewa na mabadiliko ya tabianchi, mazingira mabaya ambayo yanatokea kila wakati na mabadiliko ya spishi,'' anaongeza Dk. Kalashnikova.

Nyangumi huyo dume aliyehama alikuwamo katika kundi la nyangumi wenye nundu ambao walinaswa katika picha iliyochukuliwa kutoka kwenye meli ya utafiti pwani ya bahari ya pasifiki nchini Colombia mwaka 2013.

Katika jambo la kushangaza alionekana tena kwenye pwani hiyo mwaka 2017 na baadaye 2022 alikutwa Tanzania kisiwani Zanzibar.

Uhamaji huo wa umbali wa kilomita 13,046, haionekani kuwa ni kawaida ambao nyangumi huyo angeweza kuchukua, lakini wanasayansi wanasisitiza kuwa bado ni mrefu zaidi kuwahi kurekodiwa.

Wanasayansi wanaeleza kwamba dunia ni duara, hivyo njia fupi ni kati ya maeneo mawili kwa umbali wa mzunguko mkubwa ambao ni sehemu inayounganisha sehemu mbili kwenye duara dunia.

Matokeo ya utafiti huo yamejumuisha maelfu ya picha za nyangumi zilizowasilishwa na watafiti, waangalizi wa nyangumi na wanajamii katika tovuti ya sayansi ya happywhale.com.

Hifadhi hiyo ambayo hutumia akili mnemba kulinganisha maumbo na mifumo ya mapambo ya mkia wa nyangumi mwenye nundu na hivyo kuorodhesha harakati zao duniani kote.

Nyangumi kuonekana katika bahari ya Tanzania siyo jambo geni, bali inaelezwa kila mwaka kuanzia mwishoni mwa Julai, wanyama hao hufika hifadhi ya bahari iliyoko Mtwara kwa makundi kwa makundi wakitokea Bahari ya Kusini.

Katika kipindi hicho nyangumi kutika nchi za Afrika Kusini na Msumbiji, hukaa kwenye hifadhi hiyo mpaka mwezi Novemba.

Wanyama hao huwa na tabia ya kukaa kwenye maeneo tofauti tofauti kutegemeana na misimu inayobadilika. Hata hivyo, kwenye kila ukanda wa bahari huwa na eneo maalumu ambalo hufanya makazi yao.

Inadaiwa kuwa kwa ukanda wa Bahari ya Hindi na nchi za Afrika, mashariki Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na maingilio ya Mto Ruvuma ndiyo sehemu pekee inayowavutia wanyama hao kuishi.

Paul Maige ambaye ni Mhifadhi wa Bahari na mwongoza watalii wa ghuba hiyo, anasema kuwa sababu kubwa zinazowafanya wanyama hao wavutiwe kukaa kwenye hifadhi hiyo ni kutokana na kuwa na mazingira salama na yenye joto, tofauti na maeneo wanayotoka ambayo yana baridi.

Anasema wanapofika kwenye eneo hilo hutumia muda huo kwa ajili ya kujamiana ili waweze kuzaana.

Hata hivyo, uhamaji wa nyangumi huyo ni jambo la kushangaza kwa sababu hatoki katika nchi za kusini na badala yake anatokea bara la Amerika ya Kusini.

***BBC***

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Wanaolia Januari ni chungu, kumbukeni nidhamu ya pesa



Wazazi, walezi kumbukeni vifaa saidizi vya watoto na wanafunzi wenye mahitaji maalum ili wafurahie masomo Januari inapoanza. **PICHA: MTANDAO**

KIPINDI chenye gumzo la kila aina, kuanzia malalamiko nyumbani, kukimbia familia hadi kushtakiana kwa kudaiana fedha na mali kinaanza sasa.

Msimu huo unakaribia, ni baada ya mwezi Desemba kuendelea kuyoyoma ukifikia ukingoni mwa 2024 na kuikaribisha Januari 2025.

Ni msimu mwingine ambao wengi huuita pasua kichwa. Wazazi na walezi wanabungua bongo wakitaharuki kila wanapoona siku zinavyokimbia kuikaribisha Januari 2025.

Mwezi wa kwanza una mambo mengi mfano kama ni mpangaji iwe nyumba au eneo la biashara unawaza kudaiwa na kulipa kodi, ada au karo za shule kwa watoto ni jambo lisiloondoka kichwani, siku kuu za Noeli, mwisho na mwaka mpya, nazo wengi wanaziwaza.

Ndiyo maana Januari inaitwa majina mengi na kubwa zaidi ni mwezi mgumu unaojaa matumizi kuliko mapato.

Wapo watoto wanaoanza shule wa elimu ya awali, kuna wa darasa la kwanza na pia kidato cha kwanza.

Pamoja na hayo wapo wengine wanaorudi shuleni safari hii wakipanda ngazi mpya, alikuwa la pili anaingia la tatu.

Kadhalika kidato cha pili anaingia cha tatu, wote, wanahitaji maandalizi ya muhula mpya wa masomo unaoanza Januari 2025.

Wazazi na walezi wanapambana kununua vifaa vya shule kuanzia daftari, vitabu, sare, ada na wanaoingia kwa mara ya kwanza shule za bweni wana mahitaji makubwa zaidi.

Kwa kifupi Januari ni mwezi ambao wengine wanauona ni mgumu kwa kuwa wanaponda mali kumaliza mwaka bila kujali kuwa wana majukumu mengine mazito kuliko sherehe na ulevi ndani ya siku tatu.

Wakati Desemba inasisimua kutokana na sikukuu tatu za Chrismasi na kumaliza mwaka na kuanza mwingine mpya, wengi wanajisahau na kutoa kipaumbele hapo .

Wanapuuza suala za ada na heka heka za Januari na na hicho ndicho kisa cha kuuchukia mwezi huo.

### ANZENI KUJIPANGA

Licha ya wazazi na walezi wengi kuzungumzia kwamba Januari ni kipindi kigumu inavyoelekea hawajagutuka na kuweka mipango kwa sababu suala la elimu ya watoto si geni walilifahamu na si dharura, linalojulikana.

Wapo wanawake wanawekeza kwenye vikoba lakini pesa wanazitumia kwenye mavazi, sherehe pengine kusafiri badala ya kuiangalia Januari iliyojaa majukumu muhimu.

### ACHA KUFUJA

Jambo jingine linaweza kuwa kukosa nidhamu ya matumizi kutokutunza pesa au kuweka akiba.

Wengi wana mazoea ya kufanya matumizi mengi hata yasiyo ya lazima na inatokea kununua chochote hata kama hawakihitaji kwa wakati huo, ila kitanunuliwa kwa sababu kuna pesa mifukoni.

Kukosekana nidhamu kunajionyesha kwenye mengine mfano, wazazi au walezi wanaweza kutunza pesa ya ada au kodi ya biashara, kuanzisha biashara kama genge au mamalishe, lakini wanaposikia kuna sherehe wanabadilisha malengo na kutumia.

Mfano wakisikia harusi, mahafali, kipaimara au usafiri wa kwenda nyumbani kijijini mwisho wa mwaka wanazitoa na kupuuza mipango ya awali. Yote haya yanaponza.

Ni vyema kubadilika kwasababu wengi wanatafuta fedha kwa bidii lakini bila nidhamu ya matumizi mambo yanakuwa magumu na kusababisha kuichukia Januari.

Ni mwezi unaonekana wenye balaa wa shida. Ndiyo maana kwa wengine hawafanyi sherehe hasa harusi kwa sababu ni mgumu, na ikiwa utategemea michango ya watu kwa kiwango kikubwa. Fahamu utaikosa.

Mijadala ya kuiponda Januari na ushauri kutoka watu wengine, ipo kwenye mitando ya kijamii hata mazungumzo ndani ya jamii. Utasikia Januari ni mwezi ambao kabichi inakuwa nyama na sabuni ya magadi ni ya kila mtu.

### LA KUKUMBUKA

Kwa ujumla ili usiuone mwezi mchungu weka akiba kila wakati mwaka unavyoanza ikae benki au kwenye bidhaa pia kwenye mifugo kama kuku, mbuzi ama ng'ombe ili ukiuza upate fedha, kukwepa changamoto za kukosa karo na vifaa muhimu vya wanafunzi.

Jambo muhimu ni wewe kuweka malengo usiishi kienyeji, anza kuwa mtu wa kupanga mipango kwa kila program yako usilie eti Januari ni mwezi wa kilio.

Wazazi na walezi wajifunze kuweka akiba na nidhamu ya kutunza pesa kuliko kutumia kwa mambo ambayo si ya lazima.

Nyakati hizi katika shule za msingi za umma wazazi na walezi wafahamu kuwa ndiyo kipindi cha kuanza kufundisha mtaala mpya wa elimu ya msingi pamoja na masomo ya ufundi au amali.

Wanaoanza shule mwaka huu 2025 hawatasoma hadi darasa la saba, wataishia la sita na baada ya hapo wanaendelea na sekondari, hivyo chukua tahadhari mapema.

Kuna uwezekano mkubwa wa kuiona Januari chungu zaidi iwapo watoto wako wa familia moja watamaliza elimu ya msingi pamoja na kuendelea na ya sekondari, gharama za elimu zitaongezeka mara dufu.

Wazazi na walezi waanze kujifunza sasa kuwa hakuna sababu ya kuishi kwa mazoea kuwa mbunifu, jiongeze na usongembele.

Kwa wakazi wengi wa Dar es Salaam na ukanda wa Pwani Januari yao ngumu kwani wanakabiliana na jua na joto kali, fukuto jingi mchana na usiku. Yote hayo yanawataka kunywa maji zaidi. Wao na watoto wao walioko shuleni.

Pamoja na jua na joto, bidhaa zimepanda bei lakini kilio ni kwamba wana mifuko mitupu. Poleni lakini mwisho wa kuilalamikia Januari uanze sasa.



# Wakulima 5,400 nchini kuula

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAKULIMA wapatao 5,400 wa mikoa ya Tabora, Singida na Mwanza wanatarajiwa kupatiwa mafunzo ili kuongeza uzalishaji wa mazao na kipato.

Ni baada ya Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Shiriki la Trees For The Future kuingia makubaliano ya kuendesha mradi wa kuviwezesha vyuo vya kilimo kutoa mafunzo hayo kwa wakulima na kuboresha maisha yao.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Fredrick Mngube, akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa mradi huo, alisema utaanza kutekelezwa Januari mwakani katika mikoa hiyo.

"Mradi huu katika Mkoa wa Tabora utatekelezwa kwenye wilaya za Uyui na Urambo, Mkoa wa Singida Ikungu na Singida na Mwanza Wilaya za Magu na Misungwi," alisema.

Mngube, alisema wataanza kwa kuwafundisha wataalamu waliopo katika Chuo cha Tumbi kilichoko mkoani Tabora, Ukiruguru (Mwanza) na Mbondo (Kigoma).

Alisema kisha watafuatia wataalamu wa ugani ambao watafundishwa kuhusu bustani msitu ilivyo na kwenda kuwafundisha wakulima viongozi na kuunda vikundi vya watu 30.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa mradi huo utafanya kazi katika kata tano kila wilaya.

Alisema katika kila wilaya kutakuwa na wakulima 900, hivyo kufanya jumla yao kuwa 5,400 na kuendelea kutekeleza mradi huo kwa miaka mitano.

"Tunamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwawezesha maofisa ugani vitendea kazi kama pikipiki, sisi tutawasaidia namna ya kuwasaidia wakulima kutatua changamoto zilizopo," alisema.

Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Uendeshaji wa Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo Idara ya Mafunzo ya Kilimo na Utafiti wa Wizara hiyo, Godfrey Edward, alisema mradi huo utakuwa na mchango kwenye utekelezaji wa mipango ya wizara ya mageuzi katika sekta ya kilimo nchini.

Edward, alisema wizara hiyo imeandaa mpango mfupi wa ajenda 10 kwa lengo la kuhakikisha kilimo kinakua kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

Edward, alisema matarajio ya wizara ni kuhakikisha mipango iliyowekwa kwenye utekelezaji wa mradi huo yanafikiwa na kila pande na kwamba kinachotakiwa ni ufuatiliaji wa karibu kati yao na shirika hilo.

## Wizara kuanzisha mabaraza ya ardhi nchini

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini, amesema Wizara yake na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, zinatarajia kuanzisha mabaraza ya ardhi nchini ili kurahisisha kushughulikia mashauri kimahakama.

Sagini alitangaza mpango huo juzi Musoma Mkoa wa Mara ikiwa ni mwendelezo wa huduma za Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia mkoani humo.

"Ni kweli sekta ya mahakama imeimarisha na kuboresha sana huduma zake na tayari serikali imeliona hilo la mashauri ya ardhi kuchukua muda mrefu kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ukosefu wa mabaraza katika maeneo mengi," alisema Sagini.

Pia, alisema kwa sasa mchakato unaendelea ili yafanyiwe kazi kwa mfumo wa kimahakama.

"Lakini pia tunaamini kwamba kupitia Kampeni hii ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, ambayo inatoa huduma pamoja na elimu ya namna ya upatikanaji haki mbalimbali za kisheria bila malipo, itachangia kwa kiwango kikubwa kutatua migogoro hii katika mkoa huu wa Mara," alisema Sagini.

"Tunaamini kampeni hii itaimarisha utoaji wa huduma, ushauri wa kisheria kwa waathirika wa masuala ya ukatili wa kijinsia."

Mjumbe wa Bodi ya Kampeni hiyo ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, Lucas Malunde, alisema kampeni hiyo ni nyenzo muhimu katika kuhimiza na kuimarisha upatikanaji wa haki hususani kwa wale wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za mawakili.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Dk. Halfan Haule, aliomba Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia itumike kutatua migogoro ya ardhi na ukatili wa kijinsia katika mkoani humo.

Akizungumza kwa niaba ya mkuu wa mkoa huo, alisema kuna haja kwa serikali kufanya maboresho ya namna ya kushughulikia migogoro ya wananchi na kwamba imefika wakati sasa wa kuziruhusu mahakama kutumika kuamua migogoro badala ya mabaraza ya ardhi.

Alisema Mara unakabiliwa na migogoro mingi ya ardhi kutokana na sababu nyingi ikiwamo ya kukosekana kwa utatuzi wake kwa njia za kisheria.

Alisema hali hiyo, imesababisha kutokuwapo kwa mabaraza ya ardhi katika maeneo mengi ambayo yalikuwa na mamlaka ya kutoa uamuzi wa kisheria.

"Migogoro ya ardhi ni mingi sana, kwa hiyo changamoto hii ni vema ikafanyiwa kazi kwa sababu kuna mlolongo mrefu sana katika kupata uamuzi wa kisheria,"alisema Haule .



Liliani Saidi, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Sechelela jijini Dodoma, anayelelewa na Kituo cha Tanzania Shiriki Malezi Endelevu Kupinga Ukatili (TASHIMEKU) akipokea msaada wa madaftari kutoka kwa Ofisa Ustawi wa Jamii Dodoma, Rachel Balisidya, yaliyotolewa na wafadhili ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Kupiga Ukatili wa Kijinsia jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ashauri itungwe sheria kali kutokomeza ukatili

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kutunga sheria kali ili kukomesha vitendo vya ukatili katika jamii.

Mkurugenzi wa Kituo cha Tanzania Shiriki Malezi Endelevu Kupinga Ukatili (TASHIMEKU) Dodoma Makulu, Zawadi Mgeni alitoa ushauri huo jana kwenye maadhimisho ya tamasha la kupinga ukatili katika kituo hicho jijini hapa.

Zawadi, alisema sheria iliyopo ni ndogo na kuwa chanzo cha kukithiri kwa vitendo hivyo katika jamii.

"Nafikiri sheria ya adhabu iliyopo kwa sasa ni ndogo ndiyo maana vitendo hivyo vimekuwa vikijitokeza kila siku, niiombe serikali itunge adhabu kali ambayo itakomesha vitendo hivyo kufanyiwa watoto wa kike na wanawake," alisema.

Kwa upande wao watoto wanaolelewa kwenye kituo hicho, Lilian Said na Veis Hassan, wameiomba serikali kuwachukulia hatua wamiliki wa vituo ambao wamekuwa wakivitumia kama mradi wa kujipatia fedha na mali kwa wafadhili.

**Aliwaasa wanafunzi wasichana kujilinda na kujiepusha na vishawishi ili kutimiza ndoto zao za kupata elimu kwa manufaa yao ya baadaye.**

Walisema kuna wamiliki wa vituo hivyo wamekuwa wakiwatumia watoto hao kama mtaji wa kujipatia mali na fedha bila kujali kuwa walengwa ndiyo wana maisha duni.

Awali Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Rachel Balisidya, aliwataka wazazi na walezi kuongeza nguvu zaidi kwenye malezi ya watoto ili kuwaepusha na tamaa na kujikuta wakifanyiwa vitendo vya ukatili.

Aliwaasa wanafunzi wasichana kujilinda na kujiepusha na vishawishi ili kutimiza ndoto zao za kupata elimu kwa manufaa yao ya baadaye.

# Wanafunzi wasichana wafundishwa TEHAMA

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANAFUNZI wasichana wa shule za sekondari jijini hapa wamenufaika na mafunzo ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kubuni mifumo ya kutoa suluhisho la kero katika jamii.

Mafunzo hayo yaliyotolewa na Vodacom Tanzania kwa kushirikiana na wakufunzi kutoka Data Love Tanzania yanatarajia kuwafikia wanafunzi wa kike katika mikoa yote hapa nchini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari baada ya kufunga mafunzo hayo, Mkuu wa Kanda ya Kati wa Vodacom Tanzania, Joseph Sayi, alisema yamewafikia wanafunzi 2,600 katika mikoa zaidi ya saba nchini.

Alisema lengo lao ni kuona wanaifikia mikoa yote nchini, na kuwashawishi watoto wa kike kusoma masomo ya Sayansi.

"Mafunzo haya ni muhimu sana kwa wasichana kuanzia umri wa miaka 14 hadi 19 na kuwafanya wapende masomo ya sayansi," alisema Sayi.

Alisema wanafunzi hao wamejifunza vitu kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali za biashara kupita mitandao.

"Huu ni mwanzo tu lengo letu ni kuona kila mwanafunzi wa kike anashiriki mafunzo ya ICT ambayo huwajengea uwezo wa kutumia teknolojia kubuni njia ya kutatua changamoto za maendeleo," alisema Sayi.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Somoe Mkwachu, alisema wanafunzi hao wameonyesha uelewa mkubwa na kushindana kwenye ubunifu wa mifumo kupitia teknolojia.

Somoe, alisema baada ya mafunzo hayo, kila mmoja alikuja na wazo ambalo walibuni la teknolojia kwa ajili ya kulitatua ili kupata suluhisho.





# Radi yaua watatu ndani ya nyumba

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKAZI watatu wa Kijiji cha Kiwe, Kata ya Mawengi, Wilaya ya Ludewa mkoani hapa, wamekufa papo hapo kwa kupigwa na radi ndani ya nyumba wakati mvua ikinyesha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga aliliambia Nipashe kuwa tukio hilo lilitokea Desemba 15, mwaka huu majira ya jioni.

Kamanda Banga aliwataja waliokufa kuwa ni Sixbeth Haule (58), Emilian Mlelwa (55) na Lufina Ngailo (52).

Alisema wakazi hao walikutwa na mkasa huo majira ya saa 11 jioni kwenye nyumba ya Lufina.

"Chanzo cha tukio hili ni mvua kubwa zilizoambatana na radi ambazo zinaendelea kunyesha katika Wilaya ya Ludewa," alisema Banga.

Alitoa tahadhari kwa wananchi wasikae kwenye maeneo ambayo yana mvutano na radi kwa kuwa yanapelekea vifo.

Alisema wataendelea kutoa elimu kupitia wakaguzi wa kata na kuhimiza wananchi kuweka vikinga radi kwenye nyumba zao ili kunusuru vifo vya watu na madhara mengine.

"Kama ni nyumba ina umeme waone namna kuweka vikinga radi ambavyo ni imara ili inapopiga basi kuwe na uwezo wa kuzuia na tutaendelea kuwaelimisha wananchi waendelee kuvitumia ili kuepukana na madhara ya radi," alisema Kamanda huyo.

Vilevile, alitoa rai kwa wananchi wanapokuwa shambani na kuona dalili za mvua ni vema kuondoka na kurudi nyumbani kwa sababu maeneo hayo pia ni hatarishi kwa sababu ni ya milima.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, SACP Allan Bukumbi, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kushikiliwa kwa watu wanaotuhumiwa kumuua aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa, Christina Kibiki, aliyeuawa nyumbani kwake baada ya kuvamiwa na watu wasiojulikana usiku wa kuamkia Novemba 13, mwaka huu. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Wafanyabiashara waiangukia TRA

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imeombwa kuongeza ushirikiano na wafanyabiashara wa mjini Makambako ili kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato na kutatua changamoto zinazowakabili.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na baadhi ya wafanyabiashara hao walipotembelewa Meneja wa TRA Mkoa huo, Spacioza Owure kwa lengo la kuwashukuru na kuwakumbusha kulipa kodi kwa hiari ili kuyafikia malengo ya serikali.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara wa Mkoa huo na Nyanda za Juu Kusini 'A', Sifael Msigala, alisema ili kufikia malengo ya ukusanyaji wa kodi ni lazima pande hizo kushirikiana.

Kwa upande mwingine, Msigala aliikumbusha serikali ujenzi wa bandari kavu mjini Makambako ili kuchagiza ukuaji wa uchumi.

"Makambako ni katikati inapaswa tuwe na bandari hapa kwa sababu ukiongezeka mzunguko wa biashara, nitaendelea kuwa mteja wenu kwa sababu itakuwa ni faida kwangu na TRA, hivyo bandari kavu itatusaidia na tunahitaji zaidi ya hapo," alisema Msigala.

Akizungumzia kuhusu wafanyabiashara, alisema wanakabiliwa na matatizo ya makadirio ya kodi kuwa makubwa, matumizi ya tin namba bila ya ridhaa yao na lugha mbaya kwa baadhi ya maofisa.

"Unapokwenda TRA unaambiwa tin namba yako imetumika kwenye manunuzi haya ambayo wewe unakuwa huyatambui sasa sijui inakuwaje na elimu ya mara kwa mara inatusaidia," alisema.

Ibrahimu Mhanje, alisema ujenzi wa bandari hiyo utasaidia kupatikana huduma kwa urahisi kuliko ilivyo sasa kwa kufuata mbali na maeneo ya biashara.

**Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na baadhi ya wafanyabiashara hao walipotembelewa Meneja wa TRA Mkoa huo, Spacioza Owure kwa lengo la kuwashukuru na kuwakumbusha kulipa kodi kwa hiari ili kuyafikia malengo ya serikali.**

Meneja wa TRA Mkoa wa Njombe, Spacioza Owure, alisema lengo la ziara hiyo ni kuwashukuru walipakodi ambao kwa hiyari yao wamekuwa wakiingizia mapato bila ya shuruti.

"Kwa hiyo lazima tuwashukuru na wengi wametoa maoni, ushauri na wengine ni suala la elimu, tumewaelimisha na wameelewa," alisema Owure.

Meneja wa Mamlaka hiyo, Halmashauri ya Mji wa Makambako, Frank Tarimo aliahidi kushughulikia baadhi ya maoni na kero ikiwamo matumizi ya tin namba ya mfanyabiashara mmoja kutumia watu wengine bila ya ridhaa yake.

# Wiki ya Parachichi yaja

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKOA wa Njombe unakusudia kuanzisha Wiki ya Parachichi kwa kuwakutanisha wadau na kampuni za ununuzi ili kuliongezea thamani ya zao hilo kitaifa, kimataifa na kukuza uchumi wa wananchi.

Mpango huo ulitangazwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda wakati akifungua mkutano wa wadau wa Parachichi Mkoa wa Njombe uliokutanisha wakulima zaidi ya 1,000, taasisi, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) na Tume ya Umwagiliaji.

Sweda, alisema zao hilo linapaswa kuwekewa mkakati mzuri wa kuboresha ikiwa ni pamoja na kuandaa siku au wiki maalumu kwa ngazi ya mkoa.

"Wiki ya Parachichi itakuwa chachu ya kukuza uelewa, masoko na teknolojia bora kwa wakulima. kuanzia sasa tushirikishe wadau ili ijulikane kabisa Tanzania na nchi nyingine kwamba sisi tunashughuli yetu Njombe na wizara waijue tuna wiki hii," alisema Sweda.

Alisema wiki hiyo itasaidia kuimarisha ushirikiano kati ya wakulima, wanunuzi na taasisi kuhakikisha Njombe unaendelea kuwa kitovu cha zao hilo.

Baadhi ya wakulima, akiwemo Mariam Smalling alilalamikia tabia za madalali kulangua zao hilo kwa bei ndogo na kuomba mwongozo wa serikali kukabiliana nayo.

"Hawa wanunuzi wanunue moja kwa moja kwa wakulima, madalali wanatunyonya," alisema Mariam.

Onesmo Mwajombe, alisema miundombinu ya barabara mashambani, vipimo na wadudu ni kikwazo katika sekta ya kilimo mkoani humo.

Akizungumza kwa niaba ya wanunuzi wa parachichi, Hans Byanda, alisema wamekuwa wakikutana na vikwazoi ikiwemo kutofautiana kwa ushuru kati ya wilaya moja hadi nyingine na kukwamisha mizigo kwa muda mrefu na kuoza.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Njombe, Costatine Ibengwe, alisema wameanza kuchukua hatua kwakufanya maboresho kwenye barabara zote zenye uwekezaji.



## HABARI ZANZIBAR

# Watakiwa kupunguza migogoro kazini

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAMENEJA rasilimali watu wametakiwa kupunguza migogoro maeneo ya kazi ili kuongeza ufanisi kwa wafanyakazi.

Rai hiyo imetolewa na Kamishna wa Kazi wa Kamisheni ya Kazi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Rashid Khamis Othman wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa hao yaliyoandaliwa na Umoja wa Mameneja wa Rasilimali Watu Zanzibar visiwani hapa.

Othman, alisema migogoro sehemu za kazi inatokana na kuwapo kwa migongano ya maslahi kati ya mwajiri na mwajiriwa.

Alisema kinachotakiwa ni kufanya majadiliano kati ya mwajiri na mwajiriwa ili kusaidia kupunguza migogoro katika maeneo ya kazi.

Aliwataka waajiri kufuata sheria za kazi ikiwamo kulipa kima sahihi cha mshahara, kuwapa mikataba ya kazi na kibali cha kazi kwa wafanyakazi wa kigeni.

Othman, alisisitiza kuwa serikali haitasita kutoa adhabu kwa mwajiri atakayeshindwa kufuata sheria hiyo kama njia ya kumaliza migogoro hiyo.

Mwenyekiti wa Umoja wa Mameneja Rasilimali Watu Zanzibar, Omar Hassan Kigwama, alisema wamekutana kujadiliana namna ya kuwapa ujuzi watendaji hao kukabiliana na migogoro ya kazi.

Kigwama, aliwataka mameneja hao, kuzitumia changamoto hizo kuwa fursa za kupiga hatua katika utendaji wao wa kazi.

Akiwasilisha mada, Mchambuzi na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Profesa Khalfan Salim Suleiman, alisema migogoro ya kazi inaendelea kutokea kutokana na baadhi ya mameneja rasilimali watu kutokuwa na utaalamu wa kazi hiyo na kushindwa kutekeleza majukumu yao.

Aliwataka kuongeza utaalamu wao na kuepuka upendeleo baina ya mwajiri na mwajiriwa wakati wa kusimamia majukumu yao na kuwashauri kuweka mpango wa kuwapa motisha wanafanyakazi wanaotekeleza majukumu ipasavyo ili kuongeza hamasa.

# Mwinyi aagiza wanaokwamisha ZPDB wachukuliwe hatua

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameagiza viongozi na watumishi wa serikali kwa kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Taasisi ya Ofisi ya Rais Ufuatiliaji na Usimamizi na Utendaji Serikalini (ZPDB) wachukuliwe hatua.

Dk. Mwinyi alitoa agizo hilo jana wakati wa hafla ya maadhimisho ya miaka miwili taasisi hiyo iliyofanyika katika viwanja vya Ikulu visiwani hapa.

Alifafanua kuwa ametoa agizo hilo baada ya kupata taarifa kuwa viongozi na watumishi hawatoi ushirikiano wa kutosha kuiwezesha ZPDB kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Alisema viongozi hao na watumishi hao wanapaswa kuchukuliwa hatua bila ya kumwonea mtu kutokana na makosa hayo waliyofanya.

"Ni dhahiri kuwa mafanikio ya taasisi hii hayawezi kupatikana bila ya kuwapa ushirikiano wa kutosha. Kila mmoja ana wajibu wa kutekeleza majukumu yake na kuhakikisha nchi yetu inazidi kupiga hatua za haraka za maendeleo katika kukuza uchumi na kuimarisha ustawi wa jamii," alisema Mwinyi.

Awali, alisema wakati serikali yake inaingia madarakani aliahidi kukabiliana na changamoto zinazoathiri maendeleo na haki kwa kila mwananchi za rushwa, matumizi mabaya ya rasilimali za umma, uzembe, kukosa uwajibikaji katika utumishi wa umma, kutozingatiwa kwa sheria na kukiukwa kwa maadili ya utumishi ya umma.

Alisema katika kufanikisha dhamira hiyo, aliamua kuanzisha taasisi hiyo ili kusimamia utendaji serikalini na kutoa huduma za afya, elimu, maji, umeme, uwezeshaji wananchi kiuchumi, utamaduni, michezo na usafirishaji.

"Taasisi kama hizi zilianzishwa Tunisia, Kenya, Zambia, Rwanda, Malawi, Malaysia na Uingereza," alisema.

Alisema kutokana na mafanikio ya taasisi hiyo kwa miaka miwili iliyopita, hana shaka ya utendaji wa watendaji wake na anafahamu ni wataalamu wazoefu, wabobezi na wachapa kazi wakiongozwa na mkuu wao.


Alisema ameridhika na utoaji na usimamizi wa vipaumbele kwa sekta hizo kwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora katika elimu, miundombinu, uwezeshaji, utalii na barabara.

Aliwataka wadau, wizara, taasisi na washirika wa maendeleo kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya miradi.

Awali, Ofisa Mtendaji Mkuu wa ZPDB, Prof. Mohammed Hafidh Khalfan, alisema kuna viongozi wa serikali wanakwamisha jitihada za taasisi hiyo kwa kushindwa kutoa ushirikiano na kuzorotesha ufuatiliaji kwa baadhi ya miradi.

Khalfan, alisema viongozi hao wanajaribu kuingilia utendaji wa taasisi hiyo kwa uwazi kuwa kuhofia wanawatafutia makosa baadhi ya viongozi.

Mwakilishi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Codfrey Nyamrunda, alimpongeza Mwinyi kwa ubunifu huo wa kuweka chombo hicho kusaidia kusukuma kasi ya utekelezaji miradi ya wananchi wa Zanzibar.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, akipeana mkono na Mwenyekiti wa Tume ya Kodi Tanzania, Balozi Ombine Sefue, alipofika na ujumbe wake kupata maoni kuhusu mfumo wa kodi ulivyo na namna ya kuuboresha. **PICHA: O MR**

# Wizara, wadau kuinua kipato cha wakulima

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imesema itaendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao na kujipatia kipato.

Mkuu wa Divisheni ya Utafiti wa Mazao ya Chakula wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (ZARI), Salum Faki Hamad, aliyasema hayo wakati wa mafunzo ya usindikaji wa mbolea kwa kutumia malighafi ya kawaida ya Urea na kuibadilisha kuwa vidonge kwa wakulima wa Kisiwa cha Unguja yaliyofanyika Kizimbani Wilaya ya Magharibi 'A'.

Alisema kuwa hatua hizo ni pamoja na kuwawezesha wakulima kufahamu namna ya kutumia teknolojia ya kutengeneza mbolea ya urea (Urea Deep Placement - UDP) ili kuimarisha uzalishaji wa mazao ya chakula na kuongeza tija kwenye kilimo.

Hamad, alisema kwa kushirikiana na wizara hiyo watatoa mafunzo hayo li kuhakikisha wakulima wanapata mbolea kwa zaidi ya asilimia 30.

Alisema kuwa utafiti kuhusu mbolea hiyo umeonesha mafanikio kwenye zao la mpunga maeneo ya Unguja na Pemba.

Hata hivyo, alisema kuna changamoto ya ukosefu wa rasilimali za kutosha za kuzalisha mbolea hiyo hali inayowakwamisha wakulima kuitumia teknolojia hiyo kwa wingi.

Hata hivyo, alisisitiza umuhimu wa wakulima kuanza kutumia mbolea ya UDP kutokana na kuwa na faida kubwa za kiuchumi na uzalishaji kwa vile ina kiwango cha chini cha uyeyukaji na kuendelea kutumia kwa mimea kwa kipindi chote cha ukuaji tofauti na Urea ya kawaida ambayo huyeyuka haraka hasa kipindi cha mvua.

Washiriki wa mafunzo hayo, waliipongeza ZARI na kuahidi kupeleka mbolea zao kwa ajili ya kutengeneza mbolea ya UDP kwa matumizi ya kwenye mashamba yao.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na ZARI kwa kushirikiana Programu ya Ustahimilivu wa Mifumo ya Chakula kwa Tanzania (TFSRP) kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (WB).

Wakulima 30 kutoka maeneo mbalimbali ya Unguja, walishiriki mafunzo hayo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**KATULA GODFREY JUMBULA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index No. **S0214/0059**. Kilichotolewa na baraza la mitihani la Taifa mwaka 2018 MSALATO SECONDARY SCHOOL. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu naye. Polisi taarifa: **MGU/RB/1597/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ELIZABETH PATRICK LUBISHA,** Anatangaza kupotelewa na Cheti cha Kidato cha Nne chenye Index Namba **S2141/0015** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Secondari Ipuli Mwaka 2017. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/57363/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**TASLO CHARIDO MBUNDA,** anatangaza kupotea kwa Cheti cha Kidato cha Nne chenye Index namba **S.4891/0130/2017** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari Neno. Cheti hiki kimepotea katika Mtaa wa Mwafute jijini Mbeya. Yeyote atakayekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi **PHQ/MBE/MBE/40982/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **FADHILI NTAHENA ANYEGILE** amepotelewa na kadi ya gari yenye usajili namba **T 488 CGK** aina ya **SUZUKI VITARA** Colour **GREY.** Chasis: **JSAJTD44V00408945,** Engine: **3S5049408.** Kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/48228/2024**

## KUPOTEA KWA HATI

**Lucia DDharamsi Stppellenburg** anatangaza kupotea kwa hati ya kiwanja kilichopo Majengo Moshi. Chenye **Title No. 25570** Plot No. **30.Block 1.** Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha karibu cha polisi: **PHQ/KIL/MOS 29598/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**OSCAR GODFREY BAZORO,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye Namba za usajili **MC164DZE,** ENGINE NAMBA **156FM15AD3F82448,** CHASSIS NAMBA **LC6PCJK29P0044630.** Yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/58101/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZURIATH ABDULLAH KHAMIS** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE JINA LA **STRABAG COMPANY LIMITED** AINA YA LANDCRUSER YENYE NAMBA ZA USAJILI **DFP 6970.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU .TAARIFA YA POLISI **:PHQ/SHI//KAH/11989/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...50/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: RASHID SEIF KILAMA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA RITHA PIUS UISO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 27 Mwezi 12 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 16 mwezi DEC mwaka 2024

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**

**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...50/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: SALUM SHOMARI wa MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA JAFARI ABDALLAH MALANGE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 19 Mwezi 12 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 12 mwezi 12 mwaka 2024

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.31354 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE ANTONIA EDWARD LASWAI**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY BRAYSON TUMAINI IRIRA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be field on or before the 16 day of January 2025

Dated at Korogwe this 12th day of December 2024

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# DK. Biteko: Nyumba 15,000 zaunganishwa na gesi asilia

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Doto Biteko, amesema kuna zaidi ya nyumba 15,000 zilizounganishwa na mfumo wa gesi asilia na kwamba kwa mwaka huu wa fedha tayari nyingine 1,000 zitaunganishwa na mpango huo, akieleza kuwa kwa maoni yake ni hatua kubwa wamepiga.

Akizungumza jana alipofanyiwa mahojiano na shirika la habari BBC, Biteko alisema licha ya kwamba kuna mazingira mengine hayaruhusu kupeleka mifumo ya usambazaji gesi asilia, wala mitungi basi wasikate miti badala yake watumie majiko banifu.

Pia alisema hali hiyo itasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira na athari wanazoweza kuzipata, akieleza kuwa kuna miaka 60 hawajawahi kuunganisha kwa kiwango hicho, lakini kwa sasa kwa mwaka mmoja wamefikia hatua hiyo.

"Tunapiga hatua, tunakwenda nazo, kituo kimoja cha gasi kinahitaji zaidi ya Sh. bilioni tatu, sasa tumeshajenga tunataka hii Desemba kuongeza vingine vitafika vitano, tumeshawapa watu leseni za kubadilisha mifumo ya gesi, bajaji nyingi na magari yanatumia gesi tunapiga hatua.

"Na bado tunataka kutoa leseni kwa watu wanaosafirisha gasi ili tuweze kujenga vituo vingine mikoani, tunataka Dodoma, Morogoro na maeneo mengine tupeleke kwa ajili ya watu wanaotaka magari yao kutumia mfumo wa gasi," alisema Biteko.

***BBC***



Wananchi katika kisiwa kilichokumbwa na kimbunga nchini Msumbiji wakihama makazi yao baada ya kuharibiwa vibaya na gharika hilo, jana. **PICHA: MTANDAO.**

# Mivutano yakwamisha upatanishi DRC, Rwanda

**LUANDA, Angola**

OFISI ya Rais wa Angola Joao Lourenço imesema mivutano iliyojitokeza wakati wa mzungumzo ya upatanishi wa amani kati ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Rwanda, imekwamisha wapatanishi kufikia suluhisho la kuondoa sintofahamu iliyoko kati ya mataifa hayo mawili.

Rais wa DRC na Rwanda walipaswa kukutana katika mji mkuu wa Angola kuitikia mwaliko wa Rais wa taifa hilo, Joao Lourenço, ambaye ni mpatanishi wa Umoja wa Afrika kati ya nchi hizo mbili, ili kufikia makubaliano ya amani, lengo ambalo halikufikiwa.

„Tunaona kwamba mazungumzo ya pande tatu hayatafanyika kwa vile upande mmoja haupo,“ kilibaini chanzo kimoja.

Ilielezwa kuwa kulikuwa na matarajio makubwa kwamba mkutano ulioandaliwa na Rais wa Angola Lourenço ungemalizika kwa makubaliano ya kumaliza mgogoro.

Ilielezwa kuwa moja ya sababu zilizosababisha mchakato huo kukwamba ni Rwanda ambayo haikupeleka mwakilishi, kwa madai ya Kinshasa kukataa kufanya mazungumzo ya moja kwa moja na kundi la M23.

Kwa mujibu wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Rwanda, Olivier Nduhungirehe, mkutano huo haukuwa na sababu ya kufanyika tena kufuatia mkwamo wa majadiliano kati ya wakuu wa diplomasia.

„Tulialikwa kwenye mkutano huu kwa barua kutoka kwa msuluhishi Novemba 30, mwaka huu ambayo ilionyesha kuwa upande wa Kongo ulitoa makubaliano yake ya mazungumzo na M23 kama sehemu ya mchakato wa Nairobi. Pia tulipokea rasimu ya makubaliano ambayo pia yalikuwa na neno mazungumzo.

"Tulikuja hapa Luanda na tukashangaa kwamba Waziri wa Mambo ya Nje wa DRC alikataa kabisa wazo lolote la mazungumzo na M23, ambalo linapingana na makubaliano ya awali kwa vile lengo pekee la mkutano huo lilikuwa kusainiwa kwa makubaliano na kwamba. hakukuwa na makubaliano kati ya mawaziri kuhusu suala hili," alisema.

Msemaji wa Ikulu ya Kongo, Tina Salama, alisema wanaishutumu imani mbaya ya Rwanda. „Tangu kuanza kwa mchakato huo, hakujawa na swali lolote la kutiwa saini kwa makubaliano kuwa na masharti ya mazungumzo yoyote na M23, ambayo yana mstari mwekundu."

"Rais Tshiseked amesema mara nyingi: hatutazungumza na M23 kwa sababu haipo. Ni Rwanda ndio inahusika na mgogoro huu tunachukulia hiki kuwa kikwazo kikubwa kwa juhudi za kurejesha amani katika eneo la mashariki mwa DRC. Kulikuwa na mikutano kadhaa ya mawaziri na hii haikuwahi kujadiliwa," alisema.

# Mamia wahofiwa kufa kwa kimbunga Msumbiji

**MAPUTO, Msumbiji**

MAMIA ya wakazi wanaoishi katika kisiwa cha Mayotte ambacho kipo kwenye himaya ya Ufaransa katika Bahari ya Hindi, wanahofiwa kufariki kutokana na dhoruba ya kimbunga iliyopiga katika eneo hilo na kuharibu vibaya makazi na miundombinu mingine ya kijamii.

Kimbunga hicho kilichoanza kusababisha madhara katika eneo hilo juzi, kinaelezwa kusababisha pia waokoaji kukabiliwa na wakati mgumu katika juhudi za kuwafikia manusura wa kimbunga hicho kilichopewa jina la Chido.

Ilielezwa kuwa idadi kubwa ya nyumba kwa maeneo tofauti zimeporomoka vibaya, huku taswira kutoka Mayotte, zikionyesha matukio ya uharibifu wa kimbunga na marundo ya vifusi.

Msemaji wa Idara ya Ulinzi wa raia wa Ufaransa, Alexandre Jouassard alisema upepo mkali ulikuwa na nguvu za kipimo cha zaidi ya 200kph, na kwamba umesababisha baadhi ya maeneo yashindwe kufikika.

"Kila dakika na saa inayoyoma ina umuhimu mkubwa katika juhudi za uokozi. Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron yupo katika mipango ya kufanya mkutano wa dharura wenye lango la kutafutia ufumbuzi mkasa huu," alisema.

Shirika lenye wajibu wa masuala ya hali ya hewa la Ufaransa Meteo France lilisema kimbunga hicho ni kikubwa zaidi kuwahi kushuhudiwa katika kipindi cha zaidi ya miaka 90.

Mayotte ina wakazi wapatao 321,000 na inaundwa na visiwa viwili vikuu katika maeneo ya karibu ukiwa na ukubwa wa zaidi ya mara mbili ya Washington DC.

Kwa mujibu wa picha kutoka kwa vyombo vya habari vya ndani na Ufaransa, hali ilivyo kwa sasa ni kwamba mabaki ya mamia ya nyumba yanaonekana kutawanyika kando ya vilima, na minazi mirefu imeangukia paa za majengo, huku hospitali zikifurika maji.

Pia ilielezwa kuwa kiwango kamili cha majeruhi na uharibifu katika kisiwa hicho, ambacho kipo kati ya Madagascar na Msumbiji bado hakijafahamika. Ingawa ilibainishwa kwamba inaweza ikawa mamia ya watu au pengine ikawa elfu kadhaa.

Ilielezwa kuwa pamoja na hayo kunaweza kukawa na changamoto ya kupata takwimu halisi kwa kuwa baadhi ya familia zimekwisha fanya mazishi ya wapendwa wao.

***DW/PTR***

# KOCHA WA KENGOLD ALIA NA MABEKI, MGUNDA MENO NJE

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa KenGold, Omari Kapilima, ameilalamikia safu yake ya ulinzi kuwa haikuwa makini katika mchezo wao wa juzi dhidi ya kikosi cha Juma Mgunda, Namungo FC, na kusababisha kupoteza kwa mabao 3-2, huku wakiwa wametangulia kwa mabao mawili.

Akizungumza baada ya mechi hiyo ya Ligi Kuu, iliyochezwa Uwanja wa Sokoine, Mbeya, Kapilima alisema kufungwa kutika mchezo huo kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na uzembe wa mabeki wake, hivyo akisema ni lazima afanye marekebisho makubwa kwenye usajili kipindi hiki cha dirisha dogo.

"Katika mchezo wa leo (juzi), siwezi kusema lolote zaidi ya mabeki wangu wameniangusha. Tulikuwa tayari tunaongoza kwa mabao mawili, yamerudi na wameongeza la tatu, siwezi kusema lolote zaidi ya kusema wameniangusha, safu yote, beki wa kulia, kushoto, mabeki wawili wa kati, wote wameniangusha," alisema kocha huyo kwa uchungu.

Kapilima, beki wa kati wa zamani wa Majimaji, Prisons, Yanga na Mtibwa Sugar, alibainisha kuwa kutokana na hali hiyo ni lazima afanye mabadiliko ya kusuka safu yake ya ulinzi kwa kusajili baadhi ya wachezaji wapya kwenye kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo, huku akisema bado wana nafasi ya kubaki Ligi Kuu kutokana na wingi wa mechi walizobaki nazo.

"Bado tuna michezo 16, bado nafasi ya kubaki Ligi Kuu ipo kama tunafanya marekebisho kwenye safu yetu ya ulinzi kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

"Mabadiliko yatakuwapo, makubwa tu, siwezi kusema kama tutafumua kikosi ila kuna baadhi ya wachezaji wataongoza na kuwapisha wengine," alisema.

Kocha wa Namungo, Juma Mgunda, aliwapongeza wachezaji wake kwa kujituma na kurudisha mabao yote, hatimaye kufunga la ushindi.

"Mechi ilikuwa ngumu sana, kwa sababu sisi na wao wote hali yetu ilikuwa inafanana, hivyo mahitaji pia yalifanana, kubwa zaidi wakatutangulia kutufunga, tunashukuru tulipata mabao matatu ambayo yametupa ushindi, niwashukuru vijana wangu, haikuwa kazi rahisi," alisema straika huyo wa zamani wa Coastal Union.

Mishano Daudi na Joshua Ibrahim waliifungia KenGold bao dakika ya pili na tisa, lakini Namungo ilifunga mabao matatu kipindi cha pili, mawili ya Erasto Nyoni na moja la Fabrice Ngoy.

Matokeo hayo, yameendelea kuwabakisha KenGold mkiani mwa msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi sita, michezo 14, Namungo ikifikisha pointi 13, mechi 14, ikiwa nafasi ya 12.

# Tanzania mwenyeji mikono ufukweni

**Na Shufaa Lyimo**

TANZANIA imepata nafasi ya kuandaa mashindano ya mpira wa mikono ya ufukweni yanayotarajiwa kufanyika visiwani Zanzibar kuanzia Februari 20-25, mwakani, imethibitishwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Mpira wa Mikono ya Ufukweni, Bruno Johnson, alisema lengo la mashindano hayo ni kuwania kufuzu kucheza fainali za Mataifa ya Afrika zitakazofanyika mwakani nchini Tunisia.

Alisema mashindano hayo yatashirikisha wasichana na wavulana wenye umri chini ya miaka 17 na kwamba maandalizi tayari yameanza.

"Mpaka sasa tayari tumeanza kufanya maandalizi kuelekea kwenye mashindano hayo ambayo kwa upande wa Tanzania naamini tutakwenda kuiwakilisha vema nchi ya Tanzania," alisema Johnson.

Alisema Tanzania kupata nafasi ya kuwa mwenyeji wa mashindano hayo ni jambo la kujivunia kwani mbali na faida nyingine za kiuchumi, pia ushiriki wao utasaidia kuwatangaza wachezaji pamoja na kuwasaidia kupata nafasi ya kucheza nje ya nchi.

Mwenyekiti huyo alisema pia kupitia mashindano hayo watapata timu imara ambayo itakwenda nchini Tunisia na kuwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi siku ya mashindano hayo.

"Tunaomba Watanzania na wadau wa mchezo huu kujitokeza kwa wingi siku hiyo ili waone vipaji vitakavyokuwa vinaoneshwa siku hiyo," alisema.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, akikabidhi kitita cha Sh. milioni 10 kwa Nahodha wa Simba, Mohame Hussein ,Tshabalala', kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwa ni zawadi ya 'Bao la Mama' kwa timu hiyo kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Rais Samia amekuwa akitoa Sh. milioni tano kwa kila goli la ushindi kwa timu za Tanzania zinazoshinda kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika. **MPIGAPICHA WETU**

# Mtibwa yaendeleza vipigo Championship

**Na Adam Fungamwango**

MTIBWA Sugar, juzi ilipata ushindi wake wa tisa kwenye Ligi ya Championship kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mbeya Kwanza uliochezwa Uwanja wa Manungu Complex, Manungu, Turuani mkoani Morogoro.

Ushindi huo umeendelea kuifanya kujitanua kileleni mwa msimamo, ikifikisha pointi 29, baada ya kucheza mechi 12, ikishinda tisa, sare mbili na kupoteza mchezo mmoja.

Timu hiyo imefunga mabao 21 mpaka sasa na kuruhusu sita, ikifuatiwa na Geita Gold ambayo juzi, ikiwa ugenini Uwanja wa Majimaji, Songea, ililazimishwa suluhu dhidi ya Songea United.

Mabao ya Mtibwa Sugar yalifungwa na straika wake hatari, Raizin Hafidh, dakika ya 15 na 29, akifikisha jumla ya mabao 10 kwenye ligi hiyo na kuwa kinara wa upachikaji mabao mpaka sasa.

Baada ya kipigo hicho, Mbeya Kwanza inasalia nafasi ya sita ya msimamo ikiwa na pointi 21, kwa michezo 12 iliyocheza mpaka sasa.

Baada ya suluhu ya juzi dhidi ya Songea United, Geita Gold inafikisha pointi 27, pointi mbili nyuma ya vinara Mtibwa Sugar, huku zote zikiwa zimecheza michezo 12.

Mtibwa Sugar na Geita Gold, zote zilishuka daraja msimu uliopita kutoka Ligi Kuu.

Mechi zingine za raundi ya 12 zilizopigwa juzi ni African Sports iliyokuwa Uwanja wa TFF Centre, Mnyanjani jijini Tanga, ikilazimishwa suluhu dhidi ya Bigman FC, huku Kiluvya FC ikiitwanga TMA bao 1-0, mechi ikichezwa Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani, nayo Biashara United ikiwa nyumbani, Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Cosmopolitan.

Nafasi ya tatu kwenye ligi hiyo inashikiliwa na Stand United yenye pointi 23, Mbeya City ya nne, ikiwa na pointi 22, TMA iko ya tano ikiwa na pointi 21, Mbeya Kwanza nafasi ya sita pia baada ya kukusanya alama 21.

## ZISIKUPITE

### MUANI ATAKIWA UNITED

MANCHESTER United ina nia ya kumsajili fowadi wa Ufaransa, Randal Kolo Muani, mwenye umri wa miaka 2, kutoka PSG na huenda likawa chaguo la mkopo ambalo lina kifungu cha kumnunua jumla Januari. ***(L'Equipe)***

### NEWCASTLE KWA CHRISTENSEN

KLABU ya Newcastle United inalenga kumnunua mlinzi wa Barcelona, Andreas Christensen mwenye umri wa miaka 28, na kumuuza mchezaji huyo wa Kimataifa wa Denmark kunaweza kuruhusu klabu hiyo ya LaLiga kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Dani Olmo mwenye umri wa miaka 26. ***(Fichajes)***

### TRIPPIER KUWEKWA SOKONI

NEWCASTLE United pia inapanga kumuuza beki wa kushoto wa England, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 34, na kiungo mshambuliaji wa Paraguay, Miguel Almiron (30), ili kusaidia msimamo wao linapokuja suala la sheria za faida na uendelevu. ***(Football Insider)***

### CHUKWUEMEKA KURUHUSIWA

CHELSEA iko tayari kuwaruhusu wachezaji wa kati wa England, Kiernan Dewsbury-Hall mwenye umri wa miaka 26 na Carney Chukwuemeka (21), kuondoka kwa mkopo katika klabu hiyo Januari. ***(Mirror)***

### HALL KUREJESHWA LEICESTER

LEICESTER City inapanga kumrejesha klabuni, Kiernan Dewsbury-Hall, baada ya kumuuza kwa Chelsea katika majira ya joto. ***(Football Insider)***

### POTTER KAIKATAA WOLVES

KOCHA wa zamani wa Brighton na Chelsea, Graham Potter, alikataa nia ya Wolves mwezi uliopita huku klabu hiyo ya Midlands ikitafuta chaguo sahihi la kuchukua nafasi ya Gary O'Neil, ambaye kwa sasa ametimuliwa. ***(Guardian)***

### JACKSON NUSURA ATUE VILLA

MSHAMBULIAJI wa Senegal, Nicolas Jackson, nusura ajiunge na Aston Villa na Bournemouth kutoka Villarreal Januari 2023 kabla ya kwenda Chelsea. ***(90min)***

### PULISIC MKATABA MPYA

KLABU ya AC Milan ya Italia, inakaribia kuipata saini ya mshambuliaji wa Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 26, kwa mkataba mpya. ***(Fabrizio Romano)***

### REIJNDERS, MAIGNAN NAO

AC Milan pia wanatazamia kuongeza mkataba wa kiungo wa kati wa Uholanzi, Tijjani Reijnders na kipa wa Ufaransa, Mike Maignan kwa masharti mapya na yaliyoboreshwa**.** ***(Calciomercato)***

### MILLER ALENGWA LEVERPOOL

KIUNGO wa kati wa Motherwell na Scotland, Lennon Miller mwenye umri wa miaka 18, pia analengwa na Liverpool na anaweza kupatikana kwa pauni milioni nane. ***(Caught Offside)***

### BETO KUREJEA ITALIA

BETO wa Everton anaweza kurejea Italia Januari, huku Torino ikimtaka mshambuliaji huyo wa Guinea-Bissau. ***(Tuttomercartoweb)***

## DON… SOKA MAGA… ULAYA



# GUARDIOLA: SIFAI TENA KUWA KOCHA MAN CITY

**●●●Mimi ndiye bosi, ndiye kocha na siko vizuri, sifanyi vizuri, huo ndio ukweli, lazima nitafute...**

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola ametoa kauli ya utata kwa kusema „sifai vya kutosha" kuwa kocha wa Manchester City baada ya Manchester United kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 katika mchezo wa dabi na kusababisha kipigo cha nane katika michezo 11 kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu England.

Kiungo wa kati wa City, Phil Foden, aliishutumu timu yake baada ya mchezo, huku Bernardo Silva akisema timu yake „ilicheza kama timu ya vijana chini ya umri wa miaka 15" pale Etihad.

Lakini huku City ikishuka hadi nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu, pointi tisa nyuma ya vinara Liverpool ambao wana mchezo mmoja mkononi, Guardiola alisema kuwa sasa hafai tena kwa klabu hiyo, ikiwa ni mwezi mmoja tu baada ya kusaini mkataba wa miaka miwili.

"Mimi ndiye bosi, mimi ndiye kocha na siko vizuri," alisema Guardiola.

"Lazima nitafute suluhu, ni rahisi namna hiyo, sifanyi vizuri, huo ndio ukweli.

"Ndivyo ilivyo. Naweza kusema nini? Hatuwezi kumlaumu mchezaji huyu au yule, si hivyo. Ni msimu mgumu.

"Hatukucheza kwa ubora wetu. Sisi si bora na tunapambana kidogo. Hii ni mechi ya nane kati ya 11 kupoteza, si kawaida, kuna kitu hakipo sawa.

"Inazidi kuwa mbaya zaidi. Lazima nitafute suluhu. Hadi sasa sikuipata."

Mwenendo wa matokeo wa City sasa ndio mbaya zaidi kuwahi kutokea tangu mwaka 2003, wakati timu hiyo iliposhinda mara moja tu katika michezo 18.

Na namna walivyoshindwa dhidi ya United, huku ‚Mashetani Wekundu' hao wakifunga mara mbili dakika za mwisho kwa mkwaju wa penalti wa Bruno Fernandes na bao la ushindi la Amad Diallo, uliwaacha wachezaji waandamizi wakihoji uchezaji wa City.

"Ilikuwa ni kama timu ya vijana," alisema Foden akiiambia BBC.

"Inaonekana kuwa hadithi kwa sasa sijui nini kinatokea lakini tunazima na wanafunga mabao mawili."

Wakati huo huo, kiungo Silva alisema City walistahili kupoteza mchezo huo.

"Tulistahili kilichotokea," aliiambia Sky Sports.

"Katika kiwango hiki mchezo mmoja au miwili haina bahati. Hatuwezi kusema hii ni bahati mbaya.

"Si mchezo mmoja, ni michezo mingi hivi karibuni. Lazima tujiangalie. Unaweza kusema ohoo ni bahati mbaya, hapana. Ni maamuzi unayofanya. Leo (juzi) katika dakika za mwisho tulicheza kama vijana chini ya umri wa miaka 15." Kinachofuata kwa Guardiola na City ni mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Aston Villa ambapo watajaribu tena kurejea kwenye mstari.

HABARI MICHEZO

# Pedri ataka Barcelona waamke usingizini

**BARCELONA, Hispania**



KIUNGO Pedri amesema lazima Barcelona "tuamke kutoka usingizini" na kubadili mambo haraka kwa mwenendo wao baada ya kufungwa bao 1-0 nyumbani na Leganes juzi, Jumapili.

Bao la dakika ya nne la Sergio Gonzalez lileta tofauti kati ya timu hizo mbili huku Barca wakishindwa kushinda kwa mara ya tano katika mechi zao sita za mwisho za Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Wakati wa mbio hizo wamevuna pointi tano pekee kutoka 18 zilizotakiwa na uongozi wao kileleni mwa jedwali umeyumba. Sasa wako sawa kwa pointi na Atletico Madrid, ambao watawakaribisha wikendi ijayo, na wako pointi moja mbele ya Real Madrid, huku timu zote za Madrid zikiwa na mchezo mkononi.

"Ulikuwa mchezo mbaya, haiwezekani kuwa na furaha," alisema Pedri akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Nadhani tulianza mchezo tukiwa tumelala, tuliamka na kutengeneza nafasi, lakini hatukuwa na cheche tulizohitaji kupata bao.

"Lazima tuwe bora mbele ya lango ikiwa tunataka kuchukua pointi. Tuko kwenye mwenendo mbaya kwenye ligi na tunapaswa kubadilisha mambo."

Ulikuwa ushindi wa kwanza kwa Leganes ugenini katika LaLiga msimu huu, wakati Barca sasa wamepoteza mechi zao mbili za mwisho kwenye Uwanja wa Olympic baada ya kufungwa na Las Palmas wiki mbili zilizopita.

Barca wamebakia katika hali nzuri katika Ligi ya Mabingwa Ulaya, ingawa wameshinda michezo mitano kati ya sita katika mashindano hayo, ikiwa ni pamoja na mabao 3-2 dhidi ya Borussia Dortmund katikati ya wiki, na Pedri anatumaini wanaweza kuleta matokeo yao ya Ulaya kwenye ligi.

"Tumekuwa na mechi nyingi mfululizo, lakini si kisingizio, tunapaswa kumaliza tukiwa na imani kama hiyo tuliyofanya kwenye Ligi ya Mabingwa," aliongeza. "Ikiwa hufungi mabao katika soka, haiwezekani ukashinda."

The Blaugrana hao walimaliza mchezo kwa zaidi ya mikwaju 20, huku Lewandowski akipiga mashuti sita kati ya mashuti hayo.

Huku kocha Hansi Flick akiwa jukwaani akitumikia adhabu ya kufungiwa, msaidizi wake, Marcus Sorg, alichukua majukumu ya Mjerumani huyo.

# Pogba sasa kurejea EPL

**MANCHESTER, England**



KLABU ya Manchester City imewasiliana na Paul Pogba kuhusu uhamisho wa kushangaza wa kwenda pale Uwanja wa Etihad, kwa mujibu wa gazeti la The Independent.

Pogba kwa sasa ni mchezaji huru baada ya mkataba wake na Juventus kuvunjwa Novemba.

Kiungo huyo wa zamani wa Manchester United kwa sasa anatumikia adhabu ya kufungiwa baada ya kukutwa na hatia ya kutumia dawa za kusisimua misuli zilizopigwa marufuku michezoni, ambayo ilipunguzwa kutoka miaka minne hadi miezi 18 na anatazamiwa kumaliza Machi mwakani.

Akiwa anatazamia kupata makazi mapya, Gazeti la The Independent limeripoti kwamba Pogba amewasiliana na City kuhusu kurejea Manchester.

City wanajipanga kujiimarisha katika safu ya kiungo, ambapo kukosekana kwa Rodri kunaendelea kusababisha mambo kuwa magumu, na wanapanga kumsajili katika dirisha dogo la usajili la Januari.

Kocha Pep Guardiola anajulikana kuwa ni shabiki mkubwa wa Pogba na inasemekana anamwona mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 kama shabaha ya busara, lakini Mfaransa huyo anasita kurejea Manchester baada ya miaka sita ya misukosuko akiwa na United.

Hakika, inadhaniwa Pogba ana mashaka ya kurejea Ligi Kuu ya England kufuatia uzoefu wake katika ligi kuu ya England.

Kuhamia LaLiga, Bundesliga au Serie A kunafikiriwa kumvutia Pogba, ambaye pia amekuwa akihusishwa na miamba ya Ligue 1, Marseille.



# AMORIM AJIVUNIA USHINDI UNITED KWA MAN CITY

**MANCHESTER, England**

RUBEN Amorim amesema anajivunia wachezaji wake kwa kuamini kwamba kuna kitu kinaweza kutokea baada ya kupata ushindi wake mkubwa zaidi akiwa kocha wa Manchester United kwa kuwafunga wapinzani wao wa jiji moja Manchester City mabao 2-1 juzi kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

United walikuwa nyuma kwa bao 1-0 kabla ya Bruno Fernandes kusawazisha kwa penalti dakika ya 88 na Amad Diallo - aliyesifiwa kama "asiyezuilika" na nahodha wake - akafunga bao la dakika za mwisho.

"Ulikuwa ni mchezo wa kushangaza," alisema Amorim akiiambia BBC kuhusu mchezo huo kwenye Uwanja wa Etihad.

"Nadhani tulistahili, ilikuwa mechi ngumu sana, lakini tunaamini hadi mwisho, tulifanikiwa kufunga, tulihitaji ushindi huo, ulikuwa muhimu kwetu na kwa mashabiki wetu.

"Tulikuwa kwenye mchezo kwa dakika 90 na hiyo ni nzuri sana. Tulicheza vizuri kipindi cha kwanza, lakini walikuwa hawaamini kuwa tunaweza kushinda. Leo (juzi) ilikuwa tofauti zaidi.

"Pia ninaamini. Kisha tuna wakati wa kuweka mambo pamoja na kitu cha ajabu kilifanyika. Ilikuwa siku nzuri kwetu."

Ushindi huo ulikuwa muhimu zaidi kwa Amorim, ambaye aliwasili kutoka Sporting Club mwezi uliopita, baada ya kupoteza mfululizo kwenye Ligi Kuu.

Kuelekea mchezo huo, Man United ilikuwa imepoteza kwa mabao 2-0 kwa Arsenal na 3-2 dhidi ya Nottingham Forest.

"Mashabiki walihitaji ushindi," alisema Amorim.

"Kama sisi, lakini unaona jinsi wanavyosherehekea ni maalum. Lakini tunatakiwa kuendelea. Klabu yetu inahitaji kushinda mechi za aina hii, naelewa furaha ya mashabiki wetu, lakini tunatakiwa kuendelea.

"Tunahitaji kuboresha mambo mengi na vijana walistahili ushindi. Walikuwa ndani hadi dakika ya mwisho na hilo ni muhimu kwetu."

HABARI MICHEZO

# KIPA KAMARA APELEKWA PAMBA JIJI KWA MKOPO

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Singida Black Stars, imetangaza kumtoa golikipa wao, Mohamed Kamara, kwa mkopo wa miezi sita kwa Klabu ya Pamba Jiji.

Taarifa iliyotolea na klabu hiyo, imeeleza kuwa imeamua kumtoa kwa mkopo kipa huyo raia wa Siera Leone ili kupata muda wa kucheza, huku ikifuatilia kwa karibu maendeleo yake.

„Tumefikia uamuzi wa kumruhusu golikipa wetu (Camara), kwenda kuitumikia Pamba Jiji kwa mkopo wa miezi sita. Atajiunga rasmi na timu hiyo kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili ambalo limefunguliwa Desemba 15, mwaka huu, huku benchi la ufundi likifuatilia kwa ukaribu maendeleo yake kupitia programu yetu maalum ya ‚Loan Watch', kabla ya kumrudisha kikosini mwishoni mwa msimu," ilisema taarifa hiyo ya Singida Black Stars.

Kipa huyo tangu aliposajiliwa mwanzoni mwa msimu huu, amekuwa hapati namba mbele ya kipa Metacha Mnata, ambaye amekuwa akikaa langoni karibuni mechi nyingi za timu hiyo.

Kupelekwa kwa mkopo kwa mchezaji huyo kunaifanya Pamba Jiji kuwa na wachezaji watano mpaka sasa iliyowapata kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Timu hiyo imetangaza kuwasajili wachezaji, Deus Kaseke, Habin Kyombo, Hamad Majimengi na Cherif Ibrahim kutoka Coton Sport FC ya Cameroon.

Wakati huo huo, Singida Black Stars imepangwa kucheza dhidi ya Simba, Desemba 28, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Liti, Singida.

Kwa mujibu wa Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), awali siku hiyo ilikuwa ichezwe mechi ya Ligi Kuu kati ya Tabora United dhidi ya Simba, lakini sasa itacheza na timu hiyo, huku mchezo huo ulioondolewa sasa utapangiwa siku nyingine.

TPLB imesema maboresho hayo yamefanyika ili kuweka uwiano sawa wa idadi ya michezo kwa klabu zote katika kukamilisha michezo ya duru la kwanza, kabla ya kuendelea na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu.

## Serikali yaipa kongole Simba

Na Shufaa Lyimo

SERIKALI kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, imeipongeza timu ya Simba kutokana na ushindi iliyoupata juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, dhidi ya SC Sfaxien ya Tunisia.

Akizungumza baada ya mchezo huo wakati wa kukabidhi zawadi ya Sh. milioni 10 maarufu Bao la Mama, ikiwa ni zawadi ya Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, alisema Simba imefanya juhudi mpaka kupata matokeo ya ushindi mnono.

Rais Samia amekuwa akitoa Sh. milioni tano kwa kila bao la ushindi kwa timu za Tanzania zinazofanya vinazoshinda kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika, hivyo kwa Simba kushinda mabao 2-1 juzi, ilikabidhiwa Sh. milioni 10 baada ya mchezo huo.

„Ninaipongeza timu ya Simba kwa ushindi kwani imefanya juhudi kubwa ikaweza kuipeperusha vema bendera ya nchi yetu," alisema Msigwa.


Katibu huyo alisema hayo yametokana na kazi kubwa inayofanywa na benchi la ufundi la timu hiyo kwa kushirikiana na viongozi na wachezaji.

Alisema wachezaji wamefanya kazi kubwa na kuweza kuwapa furaha Watanzania pamoja na wadau wa soka hapa nchini.

„Ushindi huu umewapa furaha Watanzania pamoja na wadau wa soka hapa nchini, naamini michezo ijayo watafanya vizuri zaidi," alisema.

Aidha, aliwataka wachezaji hao kuongeza juhudi ili wafanikishe malengo yao kwenye mashindano hayo ya kimataifa.

MWAMBA HUYU HAPA...




Kiungo Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis, akipongezwa na wachezaji wenzake baada ya kuifungia timu yao bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Kibu ndiye mfungaji wa mabao yote mawili. **MPIGAPICHA WETU**

## Fadlu awajia juu CS Sfaxien

INATOKA UK. 24

156 na vya machungwa 100 viking'olewa na mashabiki hao.

"Fujo hiyo ilisababishwa na mashabiki wa timu ya CS Sfaxien kwa kutoridhishwa na maamuzi ya refa wa mchezo huo kuacha uendelee kwa zaidi ya dakika saba ambazo aliziongeza kama dakika za nyongeza jambo lililosababisha timu ya Simba kupata bao la pili la ushindi. Wachezaji wa ndani ya uwanja, bechi la ufundi, walikasirika, wakamfuata mwamuzi wa mchezo na kuanza kumfanyia vitendo vya kumshambulia," ilisema taarifa hiyo.

Simba ilipata ushindi kwa mabao ya Kibu Denis, yote akifunga kwa kichwa, matokeo ambayo yameifanya kufikisha pointi sita, sawa na Bravo do Maquis ya Angola ambayo juzi ikiwa nyumbani ilichapa CS Contantine ya Algeria mabao 3-2.

Pamoja na kufungwa, CS Constantine iko kwenye nafasi ya pili, nayo ikiwa na pointi sita, Simba ikiwa ya tatu kutokana na tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa, CS Sfaxien ikishika mkia, ikiwa haina pointi.

## Yanga yaanika vurugu, mateso

INATOKA UK. 24

na hasira walitaka kwenda kuwapiga wachezaji wake, lakini kwa bahati mbaya sehemu ambayo walitaka kupita ndiyo wao walikuwa wamesimama.

"Mashabiki wa TP Mazembe walikuwa wanataka kwenda vyumbani kuwapiga wachezaji wao kutokana na sare waliyoipata, kwa bahati mbaya sana sisi tulikuwa tumekaa kwenye njia ambayo ndiyo walikuwa wanataka kupita, wakaanza kutupiga sisi kwanza, tumepigwa sana, tumepigwa na chupa, mawe, viatu na kila kitu, askari walichofanya ni kutuambia tukumbatiane ili hata kama tukipigwa silaha ziishie mgongoni na si usoni au sehemu nyingine ya mwili ambayo ingeweza kuwa ni ya hatari, mpaka baadaye sana tukaja kuokolewa na askari, lakini hali haikuwa nzuri kabisa, unaweza kuona kama ni utani, hatujafanyiwa fujo mashabiki wa Yanga ila ni Watanzania, mashabiki wamefika mpakani wakawekwa tena masaa sita kwa makusudi,"alisema.

Kamwe akabainisha kuwa kunapokuja suala la kizalendo waangalie ni namna gani ya kudili nalo kwani Congo kumefanyika mambo mazito lakini ipo kimya, hakuna hata mchambuzi mmoja aliyesema.

Naye kocha wa timu hiyo, Sead Ramovic, alisema tayari ameanza kuona mwanga, kwani wakati anakuja kulikuwa na vitu vinne ambavyo vilikuwa anavifanyia kazi.

Michezo
Jumanne Desemba 17, 2024
Nipashe

## Guardiola: Sifai tena kuwa kocha Man City

UKURASA 21



CHUMA HICHO!...




Winga wa Manchester United, Amad Diallo, akiifungia timu yake bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya majirani zao, Manchester City kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Etihad juzi. **PICHA: MTANDAO**

# FADLU AWAJIA JUU CS SFAXIEN

Jeshi la Polisi lasema wang'oa viti ni mashabiki wa Watunisia hao, serikali yataka vilipwe na...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davis, amewalaumu wachezaji na benchi la ufundi la CS Sfaxien ya Tunisia kuwa chanzo cha vurugu zilizotokea juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, katika mchezo wa raundi ya tatu wa Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, Simba ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1, lakini mchezo huo ukimalizika kwa vurugu kubwa iliyosababishwa na mashabiki, wachezaji wa benchi la ufundi la CS Sfaxien ambao walionekana kutoridhishwa na muda ulioongezwa, alisema ni aibu kwa timu kubwa kama hiyo kufanya vurugu, akilitaka Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), kufanya uchunguzi na kuchukua hatua.

Fadlu ambaye alitumia muda mwingi kulizungumzia suala hilo, alisema sababu kubwa ilianza kwa wachezaji wa timu hiyo kusingizia wameumia wakati si kweli na hata zilipoongezwa dakika saba, bado waliendelea kusingizia kuumia kitu ambacho kilimfanya mwamuzi kuongeza dakika.

"Unakuwa na timu ambayo inapoteza muda kila wanapokabiliana na wachezaji wa timu pinzani, kipa wao alikuwa kinara wa kupoteza muda, mwamuzi amefidia tumepata bao, bado haitoshi, wachezaji na benchi lao la ufundi wameingia uwanjani kwenda kumshambulia mwamuzi.

"Nadhani yote yaliyotokea na vurugu zote, CAF wanatakiwa kufanya uchunguzi wao kwa kuwatumia makamisaa wao ili kubaini chanzo cha yote na kuchukua hatua," alisema kocha huyo.

Katika mchezo huo, mashabiki CS Sfaxien pia walifanya vurugu jukwaani na kusababisha kuvunjwa kwa viti huku wakiving'oa na kuvirusha uwanjani.

Wakati Kocha Fadlu alisema hayo, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imetoa taarifa ya kusikitishwa na vitendo vya mashabiki kung'oa na kuharibu viti vya kukalia watazamani katika mchezo huo.

Waziri wa Wizara hiyo, Profesa, Palamagamba Kabudi, amesema kuwa amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kuchukua hatua mara moja kwa kuwaandikia Klabu ya Simba na kuwanakili Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), ili gharama za uharibifu uliosababishwa wakati wa mchezo huo zilipwe.

Nalo Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, katika taarifa yake limesema litashirikiana na mamlaka zingine za kisheria kuona hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi ya vitendo vya mashabiki wa CS Sfaxien kufanya fujo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa wakati wa mechi yao dhidi ya Simba.

Taarifa hiyo iliyosainiwa na Kamanda Kanda Maalum ya Polisi, Jumanne Muliro, imeeleza kuwa katika fujo hizo, shabiki mmoja wa timu hiyo ya Tunisia aliumia na kupatiwa huduma ya kwanza, kabla ya kuruhusiwa, huku viti vya rangi ya bluu

INAENDELEA UK. 23

## Yanga yaanika vurugu, mateso mechi DR Congo

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imelalamika kufanyiwa vurugu kubwa baada ya mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika, hatua ya makundi dhidi ya TP Mazembe, uliochezwa Jumamosi katika Uwanja wa Mazembe, Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Akizungumza baada ya kurejea nchini kutoka DR Congo kwenye mechi hiyo iliyoisha kwa sare ya bao 1-1, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema mashabiki wa timu hiyo walipigwa na vitu mbalimbali kama chupa, mawe na viatu, wengine wakiporwa pesa zao, huku baadhi ‚wakitekwa' na kulazimishwa kuimba.

"Tumefanyiwa fujo kubwa haijawahi kutokea, mimi nimesafiri na Yanga miaka miwili, huu ni wa tatu sasa, ila mechi hii tumefanyiwa fujo kubwa sana nawaambia ndugu zangu, jamaa wamefanya vitu vingi vya hovyo, kwanza kulikuwa na vitendo vya wazi vya kishirikina, lakini sijaona hata mchambuzi mmoja wa DR Congo aliyerekodi na kuposti.

„Sisi wote, mashabiki, viongozi wetu na wachezaji tumefanyiwa fujo sana, kuna wakati mashabiki wetu walichukuliwa wakawekwa mahala wakaambiwa wapige magoti waanze kuimba, yaani walikuwa na hasira sana baada ya ile sare," alisema Kamwe.

Alisema kundi lingine la mashabiki liliwekwa kwenye jukwaa ambalo jua linapiga usoni, huku wakiwapiga marufuku wafanyabiashara kuwauzia maji.

"Mashabiki wengine waliwekwa eneo ambalo jua linapiga sana na wakapiga marufuku wasiuziwe hata maji ili kuwa tabu sana kwa sababu joto ambalo lipo Lubumbashi la sasa, hili la Dar es Salaam lina nafuu, lakini wachambuzi wao na watu wa habari wana uzalendo sana, hawajaandika, sijui ingetokea kwetu ingekuwaje. Nadhani wangerekodi na kuposti mitandaoni kuwa Klabu za Tanzania zimetesa watu."

Alisema baada ya mechi kumalizika, mashabiki wa TP Mazembe wakiwa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >